SportPesa
TZS. 499,059,740
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Naibu** Waziri alia ucheleweshaji wa fedha miradi Chato

UKURASA 3



Barca kumkosa Braithwaite hadi 2022

UKURASA 21

Jumatano Septemba 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580704
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ni zaidi ya sensa

• **Hakuna** kitakachoachwa, lengo kuwa na mipango halisi kwa maendeleo... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akibonyeza kitufe kuzindua mkakati wa uelimishaji na uhamasishaji wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**BOT YARIDHISHWA NA MWENENDO UCHUMI**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema imeridhishwa na...

UKURASA WA 4

**MSIBA WA HANS POPPE WAZUIA KESI YA AVEVA**

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva...

## Serikali yaanza kununua mahindi

UKURASA 3



## Kauli za IGP Sirro zaibua CHADEMA

UKURASA 2

**MICHEZO** MAZEMBE YAANIKA 23 WA KUIVAA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Shinyanga (SHYCOM), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi na ukarabati wa majengo chuoni hapo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ni zaidi ya sensa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NI zaidi ya sensa! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na mambo yatayoangaziwa wakati wa Sensa ya Sita ya Watu na Makazi nchini inayotarajiwa kufanyika Agosti mwakani.

Sensa hiyo mbali na kulenga kuiwezesha serikali kutambua idadi ya wananchi wake, itamulika hali ya makazi yao, kama wameajiriwa au hawana ajira pamoja na kujua hali zao kiuchumi.

Rais Samia Suluhu Hassan jana alizindua mkakati wa uelimishaji na uhamasishaji wa sensa hiyo, akiitaka Kamati ya Taifa ya Sensa kuwekeza nguvu katika kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa.

Akizindua mkakati huo jijini Dodoma jana, Rais Samia alisema Sensa ya Watu na Makazi ndiyo itakayowezesha nchi kupata takwimu sahihi zitakazoiongoza serikali kupeleka maendeleo kwa wananchi wake.

Rais alisema ili sensa ijayo ifanikiwe, Kamati ya Taifa ya Sensa inatakiwa kuweka mikakati ya kutosha kufikisha elimu kwa wananchi.

"Lazima kamati mtumie nafasi yenu kufikisha elimu kwa wananchi ili tuweze kupata takwimu sahihi zitakazotusaidia sisi serikali kufikisha huduma muhimu kwa wananchi wetu wote," alisema.

Rais Samia alisema kufanyika kwa sensa kutawezesha serikali kutambua idadi ya wananchi wake, hali ya makazi yao, kama wameajiriwa au hawana ajira pamoja na kujua hali zao kiuchumi.

"Tukipata takwimu sahihi tutaweza kufikisha huduma kulingana na mahitaji ya watu, hivyo basi lazima elimu itolewe ili kila mtu ahesabiwe bila kumwacha hata mmoja wetu nyuma," aliagiza.

Rais pia aliwataka viongozi wa serikali, vyama vya siasa na wa dini kutumia nafasi zao kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa wakati utakapofika.

"Niwaombe sana viongozi wangu wa dini kutumia nyumba zao za ibada kutoa elimu kwa wananchi ili watambue umuhimu wa kujitokeza kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi Agosti 2022.

"Sensa zilizokwisha kufanyika nchini ni tano hii ni ya sita na zote zilizopita pamoja na kuitwa za watu na makazi, hakuwahi kuhesabu makazi na kubainisha hali yake, lakini hii tunakwenda kuhesabu kila nyumba na kubainisha hali yake," alisema.

Mkuu wa Nchi huyo alisema kupatikana kwa takwimu za makazi kutaisaidia serikali kupata idadi sahihi na hali yake ili kuiwezesha kuangalia upya Sera ya Makazi Mijini na Vijijini.

"Hivi sasa tumeweka tozo ya pango la ardhi, lakini tulikuwa hatuna takwimu za idadi ya makazi nchini. Zoezi hili pia litatupa anuani za makazi hata kama mtu akikopa mkopo tutajua anatoka wapi na tunampataje," alisema.

Vilevile, Rais alisema takwimu zitakazopatikana wakati wa sensa zitabainisha aina ya nyumba kama ni ghorofa ni ghorofa ngapi na aina gani ya nyumba.

"Ninataka sensa hii ifanyike kwa haraka kwa ufanisi na kwa gharama nafuu," Rais Samia aliagiza.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022, alisema watahakikisha inafanyika kwa ufanisi na kila mtu atayelala nchini usiku wa sensa lazima atahesabiwa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema lengo la Sensa ya Watu na Makazi ni kupata takwimu sahihi zitakazotumika na serikali kutatua kero mbalimbli kwa wananchi wake, hivyo halitakuwa jambo jema kama kuna watu watakwepa kuhesabiwa.

Alisema kupata takwimu ya watu kunaliwezesha taifa kuitumia nguvukazi iliyopo kujenga na kuimarisha uchumi huku kukiwa na mgawanyo sawa wa rasilimali zilizopo.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema Sensa ya Watu na Makazi inakwenda kufanyika kipee kulinganisha na zile zilizopita.

"Sensa hii tunakwenda kutumia mfumo wa TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), hakutakuwa na karatasi kama zile zilizopita, tutatumia vishikwambi ambavyo vitawezesha kupatikana kwa matokeo ya takwimu kwa muda mfupi tofauti na ile ya karatasi ambayo majibu tulikuwa tunayapata baada ya miezi mitatu," alifafanua.

Sensa ya kwanza ya watu na makazi nchini ilifanyika mwaka 1967 kukiwa na wakazi milioni 12.313, ikifuatwa na sensa ya 1978 ambayo ilibaini Tanzania ilikuwa na wakazi milioni 17.513.

SENSA TANZANIA

Mwaka Idadi ya watu

| **Mwaka** | **Tz Bara** | **Zanzibar** | |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

## Kauli za IGP Sirro zaiibua CHADEMA

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kinakusudia kutangaza mgogoro na Mkuu wa Jeshi Polisi nchini, IGP Simon Sirro, ikiwa hataondolewa katika nafasi hiyo kwa madai kuwa anavunja sheria badala ya kuzilinda.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Benson Kigaila, alitangaza kusudio lao hilo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari.

Kigaila alidai kuwa wiki iliyopita, IGP Sirro, baada ya kurejea nchini akitokea Rwanda, aliwaeleza waandishi wa habari yale aliyojifunza katika nchi jirani hiyo.

Alisema IGP Sirro alisema Jeshi la Polisi Rwanda limekuwa likipita kwenye madrasa na ibada za watoto za Jumapili (Sunday School) kuona kinachofundishwa na kukusudia kuuleta utaratibu huo Tanzania.

"Hajatuambia kama aliwauliza Rwanda katiba yao inasemaje, hajatuambia sheria za Rwanda zinasemaje kuhusiana na suala hili. Tanzania siyo nchi iliyozaliwa leo, ina Katiba ya mwaka 1977 pamoja na upungufu wake na sheria zetu pamoja na upungufu wake zipo.

"Katiba hii (aliionyesha) viongozi wote pamoja na Sirro wameapa kuilinda, Ibara 26(1), alichosema Sirro kinakinzana na katiba hii, matamanio ya Sirro anayosema amejifunza kutoka Rwanda anataka Jeshi la Polisi liingie misikitini na kanisani kuandaa mitaala ni kinyume cha katiba.

"Ibada ya 19(2) inasema katika kueneza dini au kuendesha ibada majukumu hayo yatafanywa nje ya mamlaka ya kiserikali.

"Ibara 19(3) inasema kuingilia uendeshaji wa dini maana yake kutavuruga umoja wa kitaifa na kutahatarisha maadili ya jamii na imani ya jamii," alisema.Kigaila alihoji sababu za kile alichokiita 'wengine wakivunja sheria wanakamatwa lakini Mkuu huyo wa Jeshi la Polisi akivunja hakamatwi kama wahalifu wengine'.

"Kwa nini aendelee kuwa madarakani na analipwa na kodi za Watanzania? Katiba ibara 26(2) tuna wajibu kuhakikisha kwamba sheria na katiba zinahifadhiwa na kulindwa.

"Wito wetu kama chama, taasisi za vyombo vya habari, taasisi za dini, vyama vyote vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali na Watanzania tusimame kuhakikisha Katiba na sheria zinalindwa na watawala waliopo," alisema.

Pia aliyataka mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya siasa kusimama pamoja kuitaka mamlaka ya uteuzi wa IGP Sirro aondolewe kwenye nafasi hiyo kwa madai anaharibu Jeshi la Polisi na kulifanya liwe chombo cha kuvunja sheria badala ya kuzilinda.

Kigaila alisema endapo hataondolewa katika nafasi hiyo, watatangaza mgogoro naye kwa msingi kwamba anavunja katiba na sheria.

Kigaila alisema ndiyo maana wanataka kuwapo wa katiba mpya ili watu wa namna hiyo wanaoweza kuikanyaga wasitokee na endapo watajitokeza waadhibiwe mara moja.

"Hatuwezi kuwa na viongozi wa namna hii ambaye anaamka asubuhi anatamka anachotaka baadaye anatembea akiwa huru, tuwe na katiba ambayo akitokea kiongozi anaivunja madhara yake anayapata palepale," alisema.

Akizungumzia kauli ya IGP Sirro kuhusu watu wenye viashiria vya ugaidi aliyoitoa hivi karibuni, Naibu Katibu Mkuu huyo alihoji viashiria vya ugaidi.

"Unaweza kumwona mtu ukasema huyu ana viashiria vya ugaidi? Sirro anataka kujifanya kama nabii, kama mtabiri kwamba anaweza kukutana na mtu anavyotembea akasema una viashiria vya ugaidi, ukachukuliwa.

"Sheria ya ugaidi ipo lakini haijasema kuna watu wana viashiria vya ugaidi, anataka Watanzania waanze kutuhumiana kwa viashiria vya ugaidi ambavyo havijafafanuliwa na sheria, wampelekee atakaa nao awarekebishe, amesharekebisha watu gani?" Kigaila alihoji.

Nipashe ilipomtafuta IGP Sirro kuhusiana na kauli hizo za CHADEMA, aliomba atafutwe Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, ili kuzizungumzia.

Gazeti hili lilimtafuta Misime ambaye alisema Jeshi la Polisi haliwezi na halina utaratibu wa kulumbana na yeyote ambaye anaamua kutafsiri aonavyo jambo aliloambiwa au alilosikia.

Hata hivyo, alisema jeshi hilo linaendelea kusisitiza yale lililojifunza kutokana na ziara iliyofanyika nchi jirani ya Rwanda juu ya namna bora ya kufuatilia yanayofundishwa katika shule za dini, yatawasilishwa kwa viongozi na wadau wengine na kama kuna jambo likionekana linafaa na litaendelea kudumisha haki, amani na utulivu katika nchi, litawekewa utaratibu wa utekelezaji. Hali kadhalika, Misime alisema kama kuna jambo likionekana halifai, ndiyo mwisho wake kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa, hivyo inajifunza kutoka kwa majirani.

"Ikumbukwe ufuatiliaji wa yanayoendelea maeneo yote, yawe ya kisiasa, kidini, kibiashara, kijamii kila nchi imejiwekea utaratibu wake ili kutotoa mwanya kutumika kama mwavuli wa kupanga na kutenda uhalifu utakaosababisha amani na utulivu kutoweka.

"Nani asiyefahamu baadhi ya watu walishaitwa baada ya taarifa na malalamiko kutolewa na wakahojiwa kuhusu waliyofundisha na kusema huo nao ni ufuatiliaji wa kuona kama kuna makosa ya jinai yaliyotendeka au uhalifu unaopangwa?

"Nani asijejua malalamiko yalishawahi kutolewa kuhusu baadhi ya nyumba za ibada kutumika kwa mazoezi usiku na ufuatiliaji ukafanyika?

"Pia malalamiko yamewahi kutolewa kuwa baadhi ya nyumba za ibada kuna ibada zinaendelea usiku wa manane na kusababisha usumbufu kwa wengine.

"Pia malalamiko yalishatolewa kuna watoto wadogo sana wameonekana wamekusanywa katika nyumba fulani na ufuatiliaji ukafanyika na ikabainika kwa umri wa watoto hao na katika mazingira waliokuwa wakiishi kwa minajili ya kufundishwa dini hayafai na wala hao watoto hawakuwa wamefikia umri wa kutenganishwa na wazazi wao na wala hawakuwa wanapatiwa elimu iliyokuwa wanastahili kupatiwa kwa mujibu wa sheria," alifafanua.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaanza kununua mahindi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NEEMA imetua kwa wakulima wa mahindi baada ya serikali kuanza kununua tani 90,000 kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB).

Ununuzi huo umeanza baada ya serikali kutoa Sh. bilioni 50 ili kunusuru soko la mahindi ambalo lilionekana kusuasua hivi karibuni.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema NFRA itaanza kununua kwenye mikoa saba kwa bei ya Sh. 500 kwa kilo na CPB itanunua kwenye mikoa sita kulingana na bei ya soko.

Waziri alitaja mikoa saba ambayo NFRA itaanza kununua mahindi hayo kuwa ni pamoja na Ruvuma, Rukwa, Njombe, Songwe, Mbeya, Katavi na Iringa na CPB ikinunua mikoa ya Rukwa, Katavi, Njombe, Songwe, Dodoma na Manyara.

Alibainisha mwaka huu zimezalishwa tani milioni sita za mahindi huku ziada ikiwa mara mbili ya uzalishaji uliofanyika kwa mwaka uliopita huku nchi za Zimbabwe na Zambia zikitajwa kuzalisha kwa wingi nafaka hiyo.

"Mwakani bei inaweza kupanda lakini kwa kuwa kuna mikoa inaongoza kwa uzalishaji nchini kama Ruvuma ukifuatiwa na Rukwa, bei ni ndogo sana wakati Mkoa wa Katavi, Songwe zikiwa chini zaidi hali inayopelekea mkulima kushindwa kupata fedha za kujikimu na kujiandaa kwa msimu ujao," alisema.

Waziri huyo alisema mahindi hayo yatanunuliwa kupitia Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) au vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa na kwa wakulima wadogo kwa magunia yasiyozidi 300 au tani 30.

"Tunataka rekodi ya kila mkulima aliyelima mahindi yanunuliwe na fedha zilizotolewa na serikali zitumike kama ilivyokusudiwa.

"Baada ya zoezi hili kufanyika, wizara itafanya ufuatiliaji kwa viongozi wa mikoa ili kupata taarifa na namna mgawanyo wa ununuzi ulivyofanyika kwenye mikoa tajwa," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Milton Lupa, alisema wanakwenda kununua nafaka hiyo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwenye mikoa ya Ruvuma, Songwe, Njombe, Katavi na Rukwa kupitia AMCOS na wakulima waliosajiliwa.

"Wananchi watulie tutanunua mahindi, wapunguze vurugu kwa kuwa tutafuata utaratibu uliowekwa, tunawahakikishia tutawafikia wakulima wenye kipato cha chini wenye mahindi yanayokidhi vigezo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu CPB, Dk. Anselm Mushi, alisema watanunua mahindi hayo kama walivyoelekezwa na wizara na kwamba wameshaanza kutafuta masoko nje katika nchi za Kenya, Sudan Kusini, Comoro, Burundi na Rwanda.

## Mabula alia kuchelewa fedha miradi NHC Chato

**Na Munir Shemweta,** CHATO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekagua miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Chato mkoani Geita na kusikitishwa na kusuasua kwa utekelezaji wake kunakosababishwa na ucheleweshaji wa fedha.

Dk. Mabula alikagua miradi mitatu inayotekelezwa na NHC ambayo ni mradi wa mnada wa mifugo Buzirayombo wenye thamani ya Sh. bilioni 4.8, ujenzi wa shule maalum ya Mbuye wenye thamani ya Sh. bilioni 5.14 pamoja na mradi wa nyumba 20 za watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda - Chato wa thamani ya Sh. bilioni 1.139.

Akizungumza baada ya kukagua miradi yote mitatu jana, akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Geita, Dk. Mabula alisema miradi hiyo ni muhimu na inapaswa kukamilika kwa wakati ili ianze kutumika.

"Haitakuwa na maana serikali kuwekeza fedha nyingi kwenye miradi ya mnada wa mifugo, shule maalum na nyumba za watumishi wa sekta ya afya na kuachwa bila kukamilika jambo ambalo halitaleta maana," alisema.

Meneja wa NHC Mkoa wa Kagera, Maneno Mahenge, alimwambia Naibu Waziri kuwa NHC imekuwa likisuasua kutekeleza kwa kasi miradi katika wilaya hiyo kutokana na kutopatiwa fedha za miradi kwa wakati.

Alisema shirika hadi sasa limetumia takribani Sh. bilioni 1.02 kwenye mradi wa mnada wa mifugo, Sh. milioni 985 katika Shule Maalum ya Mbuye na Sh. milioni 275 kwa ajili ya utekelezaji mradi wa nyumba za watumishi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda na fedha zote hizo bado halijalipwa.

"Kama taarifa hazifiki kwa wakati basi miradi itasimama na haileti picha nzuri na ukiangalia hapa tatizo kubwa ni mawasiliano na taarifa zikiwapo basi kazi itaenda vizuri," alisema.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**WAHARIBIFU WA MINADA KWA NJIA YA MTANDAO**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mara kwa mara inaendesha minada kwa njia ya mtandao yaani **Online Auctions** kwa mizigo iliyoshindwa kukamilisha taratibu za forodha na kupitisha muda kwa mujibu wa sheria ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Katika ushiriki wa minada hii, Mamlaka ya Mapato inapenda kuutaarifu umma kwamba, wapo washiriki wa minada ambao wanashinda na kuacha kulipia bidhaa husika kwa mujibu wa vigezo na masharti vilivyowekwa katika uendeshaji wa minada hivyo wametenda kosa la kuharibu mnada kwa makusudi.

Hivyo, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatoa wito kwa washiriki hao kuacha kitendo hicho maramoja kwani ni kosa kisheria, na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakaebainika kujihusisha au kwenda kinyume na masharti na taratibu za mnada kama sheria inavyoelekeza

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**KAMISHNA WA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA**

216454802

# Msiba wa Hans Poppe wakwamisha kesi ya Aveva

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva, ameshindwa kuendelea kujitetea kwa sababu mshtakiwa mwenzao, Zackaria Hans Poppe, kufariki dunia.

Kesi hiyo yenye mashtaka saba, ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka, ilikuja jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa ajili ya washtakiwa kujitetea.

Wakili wa Utetezi, Benedict Ishabakaki, aliiarifu mahakama mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwamba mshtakiwa Hansp Pope amefariki dunia, hivyo aliomba kesi iahirishwe ili waende kwenye mazishi.

Hakimu Simba alikubali kuahirisha kesi hiyo hadi Septemba 22, mwaka huu na kumwamuru Wakili Ishabakaki kuwasilisha hati ya kifo ili mahakama iombe kumuondoa marehemu katika kesi hiyo.

Mbali na Aveva, washtakiwa wengine ni aliyekuwa makamu wake, Godfrey Nyange maarufu Kaburu na Hans Poppe aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ambaye alifariki dunia Septemba 10, mwaka huu jijini Dar es Salaam na anatarajiwa kuzikwa leo nyumbani kwao, mkoani Iringa.

Katika mashtaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

Pia Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja walighushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva kitu ambacho si kweli.

Aidha, Aveva anadaiwa katika benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 na pia anadaiwa kuwa katika Benki ya Barclays, Mikocheni mkoani Dar es Salaam, alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na Hans Poppe wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba si kweli.

Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577




Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, Saad Mtambule (katikati), na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Happiness Laiza (kulia kwake), wakikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni 292,7 kwa vikundi vya vijana, watu wenye ulemavu na wanawake, wilayani humo jana, fedha za mikopo isiyo na riba. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# BoT yaridhishwa na mwenendo wa uchumi

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema imeridhishwa na utekelezaji wa sera ya taifa ya fedha pamoja na mwenendo wa uchumi wa ndani na wa dunia kwa Julai na Agosti, mwaka huu, kutokana na kuongezeka kwa ukwasi katika tasnia ya benki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na benki hiyo, uwapo wa ukwasi wa kutosha katika kipindi hicho kwenye tasnia ya benki umejidhihirisha katika viwango vya riba katika masoko ya fedha ambavyo vimeendelea kubaki kati ya asilimia tatu hadi tano.

Pia taarifa hiyo ilisema mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa kwa asilimia 4.1 kwa mwaka ulioishia Julai, kutoka asilimia 3.6 kwa mwezi uliotangulia.

"Kamati imebaini kuwa ukuaji wa uchumi wa dunia unaendelea kuimarika licha ya janga la corona, japo kwa kasi ndogo na unatarajiwa kuendelea kuimarika siku za usoni. Mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar kwa robo ya kwanza ya mwaka 2021, ulikuwa wa kuridhisha.

"Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 4.9, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, uchukuzi, kilimo, uzalishaji viwandani na uchimbaji wa madini. Uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia 2.2, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020," ilisema taarifa hiyo,

Kuhusu mfumuko wa bei, taarifa ilieleza kuwa umeendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia tatu hadi tano sawa na malengo ya kitaifa na vigezo vya mtangamano wa kikanda huku sekta ya utalii ikiendelea kukabiliwa na vikwazo vinavyotokana na corona wakati mauzo ya dhahabu yakitajwa kuongezeka kufikia dola za Marekani bilioni tatu kwa mwaka ulioishia Julai, 2021.

Akiba ya fedha za kigeni imetajwa kuendelea kubakia katika viwango vya kuridhisha na kufikia dola za Marekani bilioni 5.5 na kwamba kiasi hicho kinatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa zaidi ya miezi sita, sawa na lengo la nchi na makubaliano ya jumuiya za kikanda.

"Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikua kwa asilimia 11 kwa mwaka ulioishia Julai 2021, ukiwa ndani ya lengo la ukuaji wa wastani wa asilimia 10 kwa mwaka 2021/22, mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka, japo kwa kasi ndogo ya asilimia 4.1," ilibainisha taarifa.

## Aomba aachiwe kesi dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa pili wa utetezi, mfanyabiashara Sara Daudi Munuo (47), anayekabiliwa na wenzake wanane dhidi ya kesi ya kuingiza dawa za kulevya aina ya cocaine, kilo tano amedai mahakamani siku ya tukio alifika jijini Dar es Salaam baada ya kuandikiwa rufani kutoka Hospitali ya KCMC kwenda Muhimbili.

Kadhalika, amedai kuwa alifikia nyumbani kwa rafiki wa dada yake Mwanaidi Mfungo, ambaye pia ni mshtakiwa wa kwanza kwenye kesi hiyo. Munuo alitoa ushahidi wake wa utetezi juzi katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi chini ya Jaji Isaya Arufani.

Akiongozwa na Wakili wa utetezi Hajira Mungura, shahidi alidai kuwa Mei 31, 2011 alifika jijini Dar es Salaam akitokea Moshi, mkoani Kilimanjaro baada ya kuandikiwa rufani ya maradhi ya moyo na uzazi kutoka KCMC.

Akifafanua ushahidi wake, alidai kuwa kabla ya kufika jijini, Mei 28,2011 alimpigia simu Mfungo ambaye alifahamiana naye kwa kuwa ni rafiki wa dada yake Janeth Munuo, walifika pamoja Moshi kwenye msiba wa baba yake mzazi mwaka 2005.

"Nilimuuliza Mwanaidi kama yuko jijini alinijibu yupo, nilimjulisha lengo la safari yangu kwenda Muhimbili na kwamba nitafikia kwake, nilipofika Ubungo standi kuu ya mabasi, nilichukua taksi na alimwelekeza dereva kwa njia ya simu anipeleke Mbezi Beach na namna ya kufika kwake," alidai na kuongeza.

"Nilipofika nilipokelewa, nilimkuta mwenyeji wangu na wanaume wawili (kwa sasa mshtakiwa wa tatu na wa nne) walikaa sebuleni wakiangalia runinga, kwa kuwa nilikuwa na uchovu na maumivu ya maradhi yangu, niliomba mahali pa kupumzika, nilionyeshwa chumba," alidai Munuo.

Aliendelea kujitetea kuwa aliamshwa kwa chakula cha usiku na baadaye alirejea chumbani kulala.

Hata hivyo, katikati ya usingizi aliona mtu akimuamsha kwa nguvu, aliposhtuka aliwaona watu wengi wakiwa ndani ya chumba alichokuwa amelala, wakamlazimisha atoke nje huku wakimsukuma.

Alidai kuwa watu hao walikuwa 10 wakiwamo wanawake wawili na wanaume wanane.

"Nilipotolewa nje niliwakuta vijana wawili na mshtakiwa wa kwanza wakiwa wamelala katika baraza ya nyumba hiyo.

Akiendelea na utetezi wake shahidi alidai kuwa, wale watu walimnyanyua mshtakiwa wa kwanza na wakaingia naye ndani na baadaye walimrudisha nje.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Anthony Karanja, Ben Ngare, Almas Said, Yahaya Ibrahim, Aisha Kungwi na Rajabu Mzombe, ambao walisomewa mashtaka yao kwa mara ya kwanza 2011 mpaka sasa ni miaka 10, wakiwa mahabusu.

# Bei ya pamba yapaa kwa 58%

**Na Happy Severine, MEATU.**

MKOA wa Simiyu ambao ni kinara wa uzalishaji pamba, umetangaza kupanda kwa bei ya zao hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amesema bei ya pamba imepanda kutoka Sh. 1,050 kwa kilo ambayo ilitangazwa na serikali kupitia Bodi ya Pamba (CBT) hadi Sh. 1,800.

Akizungumza na wakazi wa Kata ya Kisesa katika Kijiji cha Mwaukoli, Kafulila alisema kwa mwaka huu bei imepanda kuliko misimu mingine yote tangu zao hilo, limeanza kuzalishwa nchini.

Alisema kuwa kwa mara ya kwanza wakulima wa pamba mkoani Simiyu wameuza pamba yao kwa Sh. 1,800, huku akieleza kuwa mipango ya serikali ni kudhibiti mbinu chafu zilizokuwa zikifanywa na wanunuzi wa pamba.

" Bei nzuri ya pamba nchini mwaka huu ni matokeo ya uongozi thabiti serikali, wanaodhani sababu ni ongezeko la bei kwenye soko la dunia pekee hawako sahihi," alisema Kafulila.

"Watu wanapaswa kufahamu kuwa bei ya soko la dunia kwa sasa ni Dola senti 90, hata mwaka 2018, 2013 bei ilikuwa hiyo hiyo kwenye soko la dunia, lakini kwa bei ya ndani haijawahi kufikia kiwango cha Sh. 1,800 kwa kilo," alisema Kafulila.

Baadhi ya wananchi katika kijiji hicho walikiri kuuza pamba yao kwa Sh.1,800 kwa kilo, huku wakibainisha kuwa haijawahi kutokea bei ya pamba kupamba kwa kiwango hicho.

Wananchi hao waliipongeza serikali kwa kusimamia suala la bei ya pamba ambayo imesababisha wengi wao kuhamasika kulima zaidi zao hilo katika msimu mpya wa zao hilo mwaka huu.

" Ni kweli Mkuu wa Mkoa kama ambavyo ulisema, hapa kwenye kijiji chetu wengi tumenunua kwa bei hiyo mpya, tunaishukuru sana serikali, tunaiomba bei hii iendelee kuimarika, lakini isishuke kutoka hapa, tunamshukuru Rais Samia amesababisha wengi tuwe na matumaini na pamba," alisema John Maduhu

Mkoa wa Simiyu katika msimu wa mwaka 2021/22 umepanga kuzalisha tani 500,000 na mkakati huo umelenga kuwawezesha wakulima kupata pembejeo kwa wakati.

# 'Watu wagombanie mgonjwa, sio maiti'

**Na Halfani Chusi**

JUMUIYA ya Akhlaaqul Islam (JAI) imewataka watu kuwa na utaratibu wa kugombania kumhudumia mgonjwa na sio maiti ili kuongeza nguvu ya kunusuru uhai wa mtu.

Amiri Mkuu Tanzania, Yahya Ally Masao, alitoa rai hiyo katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala mkoani Dar es Salaam alipozungumza na Nipashe wakati jumuiya hiyo ilipotembelea hospitalini huko kwa ajili ya kutoa misaada kwa wagonjwa.

Masao alisema malengo ya jumuiya hii ni kunyanyua utu na ubinadamu ili ustawi kwenye jamiii katika kuwahudumia wagonjwa waliokosa ndugu.

"Hii jumuiya ni ya kidini na lengo kubwa lake ni kuwahudumia wagonjwa waliokosa ndugu katika hospitali za serikali.

"Wagonjwa ambao ndugu hawana uwezo wa kuwahudumia, wagonjwa ambao ndugu hawana taarifa, wagonjwa ambao ndugu wamewakimbia hospitalini baada ya kuishiwa, wagonjwa ambao wameletwa na polisi, pia katika kuwatolea damu wagonjwa ambao wana mahitaji ya damu kama wajawazito, watoto, ajali na matatizo ya kansa na unakuta hawana msaada.

"Pia kuwasaidia wagonjwa dawa ambazo zimekosekana hospitalini, kuwapatia huduma za vyakula, maji na kifungua kinywa, pia kuwahudumia wagonjwa ambao wameletwa na polisi pasipo ndugu zao kujua pamoja na kuwasaidia wagonjwa kuwaunganisha na ndugu zao hasa wale wagonjwa ambao wana ndugu ila ndugu zao hawajapata taarifa yoyote.

"Na tunafanya haya kwa kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii hospitalini kwa kibali kilichotolewa na Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI.

"Kwa sasa tunaangalia mbali zaidi tuweze kufikisha huduma hii kwa baadhi ya mahabusi na wafungwa walioopo gerezani ambapo bado tunasubiria majibu Wizara ya Mambo ya Ndani (ya Nchi)," alisema.

Alivitaja vikwazo kadhaa ambazo kama taasisi wamekuwa wakikumbana nazo na kuomba baadhi ya wadau watakaoguswa kuwaunga mkono.

"Hii ni kazi ya Mungu, tunafanya kazi hii, hatutegemei malipo bali malipo yetu ni kesho kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, lakini tunakumbana na vikwazo katika kazi hii ikiwamo vyanzo vya kipato ni hafifu kutokana na kuwa wachangiaji ni wanajumuiya wenyewe pamoja na misikiti, watu na taasisi mbalimbali.

"Tuna kikwazo cha usafiri katika kuyatekeleza majukumu mbalimbali, kwa mfano, mgonjwa ameruhusiwa, inakuwa kazi kweli kumrejesha makwao.

"Pia mgonjwa anapopata rufani hospitali kukiwa na uhaba wa ambulance (gari la kubeba wagonjwa), inakuwa ni shida.

"Yote haya yapo kwa watoa huduma wetu Tanzania nzima, pia tuna uhaba wa fedha kwa ajili ya vifaa tiba kwa wagonjwa tunaowahudumia kama vile dawa, lishe na huduma mbalimbali kwa wagonjwa," alisema.

Alitoa wito kwa jamii kungana na jumuiya hiyo kusukuma gurudumu hilo la kuhudumia wagonjwa wasio na ndugu.

Kiongozi huyo wa jumuiya alisema yeyoye atakayeguswa na hili kwa lolote lile awasiliane na mweka hazina JAI.

Mohammed Chunga, Mjumbe wa JAI, alisema kwa sasa wanaisubiri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kujibu barua ya ombi lao la kuhudumia wafungwa na mahabusi walioko magerezani hususani kinamama kwa kuwapa taulo za kike na mahitaji mengine ya kiafya.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya wagonjwa hospitalini huko ambao wanahudumiwa na jumuiya hiyo, akiwamo Frank Mruanda aliyeishukuru jumuiya hiyo kwa kumhudumia kwa zaidi ya wiki mbili.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, akimjulia hali mtoto aliyejeruhiwa kwenye ajali ya basi mkoani Kagera anayeendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Bukoba, jana. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

# Waziri ambana mmiliki basi lililoua na kujeruhi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Maendeleo ya Jamii), Mwanaidi Khamis, amemwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera kuhakikisha wanamtafuta na kumpata mmiliki wa Kampuni ya Fikosh ambayo inamiliki basi lililopata ajali na kusababisha vifo vya watu watano inalipa gharama.

Kadhalika, katika ajali hiyo abiria zaidi ya 30, walijeruhiwa.

Agizo hilo lilitolewa na Naibu waziri huyo baada ya kutembelea majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera na kuelezwa kuwa tangu ajali imetokea, mmiliki wa kampuni ya basi lililosababisha ajali, hajawaji kufika hospitalini hapo kuwajulia hali majeruhi hao, ambao baadhi yao wamekatwa mikono.

"Inasikitisha, nasikia mhusika hata kufika kuwajulia hali wagonjwa ameshindwa, naagiza afuatiliwe kwa haraka na aweze kuwahudumia waliopata majeraha na wahudumiwe kikamilifu," alisema na kuongeza:

" Na pia naagiza tena, hospitali endeleeni kuwapatia huduma majeruhi hawa, ili wapone, maana majengo haya yapo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi."

Mmoja wa majeruhi wanaondelea na matibabu katika hospitali hiyo, Nobert Philbert, ambaye amekatwa mkono wa kushoto, alisema kuwa tangu ajali hiyo imetokea ni takriban siku tisa sasa, na kwamba wamekuwa wakijigharamia wenyewe matibabu, lakini wameishiwa fedha na kuomba serikali kuwasaidia.

"Mimi na familia yangu tumekuwa tukitafuta gharama za matibabu wenyewe, wakati mwingine tunaomba misaada kwa watu, lakini tunakoelekea hatutaweza kuendelea kupata fedha, na mimi kama mnavyoona nimekatwa mkono hata nikikopa sina tena uwezo wa kufanya kazi na kuingiza kipato, ili nilipe madeni baada ya kuruhusiwa," alisema Nobert.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Msereta Nyakiroto, ambaye ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa, alimweleza naibu waziri huyo kuwa majeruhi hao wanaendelea kupatiwa matibabu na hali zao zinaendelea vizuri, na kuahidi kulifanyia kazi haraka agizo walilopewa.

Basi la kampuni ya Fikosh lenye namba za usajili T710 BXB ambalo hufanya safari zake kutoka mkoani Kagera kwenda mkoani Mwanza, lilipata ajali Septemba 05, mwaka huu, wakati likitoka mkoani Mwanza na kusababisha vifo vya watu watano na majeruhi zaidi ya 30 .

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mawaziri chapeni kazi

**JUMAPILI**, Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya mabadiliko madogo ya mawaziri, huku akifanya mabadiliko ya kimuundo kwa kuiondoa Idara ya Habari (Maelezo) kutoka Wizara ya Habari na kuipeleka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia.

Kwa mawaziri watatu walioteuliwa na kurejea kwenye uwaziri January Makamba (Nishati), Prof. Makame Mbarawa (Ujenzi na Uchukuzi) na Ashatu Kijaji (Habari, Teknolojia na Mawasiliano), wanakabiliwa na mtihani mgumu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Rais Samia alisema hajaweka nukta bali ameweka koma kwa kuwa bado anaendelea na mabadiliko ya watendaji mbalimbali, ambao wako chini ya mamlaka yake ya uteuzi, ikiwa ni namna ya kutuma salamu kwa wateule kufanyakazi kwa bidii na kufikia malengo tarajiwa ya kuhudumia umma.

Alisema wateule wasitarajie kwa maumbile na malezi yake wamuone akifoka, na kwamba hatafanya hivyo kwa kuwa anafanyakazi na watu wazima wanaojua jema na baya na ni imani yake wanapozungumza wanaelewana na kila mmoja anajua wajibu wake, na pale itakapomlazimu kufoka atafoka kwa kalamu.

Aidha, alisema amejichagulia njia yake mwenyewe na anachokitaka ni serikali kuendeshwa kwa matendo makali kwa kutoa huduma muhimu kwa wananchi.

Pia, rais aligusia suala la machinga ambalo ni tatizo kubwa kwa miji na majiji , huku akiwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya kuwapanga badala ya kuwabughudhi.

Ni muhimu wateule wakatekeleza wajibu wao kwa kuhudumia wananchi kwa kuwa msingi wa yote ni kuwatumikia walipakodi pamoja na utatuzi wa kero zao.

Tunampongeza Rais kwa kusikia kilio cha vyombo vya habari nchini kwa kuunganisha vyombo vya magazeti, redio, TV na digital kusimamiwa na wizara moja, tofauti na awali.

Tasnia ya habari tuna matarajio makubwa kwa Waziri Dk. Kijaji, kwa kuwa maumivu ya kufungiwa kwa chombo cha habari ni makubwa na haiathiri chombo husika bali waajiriwa na wategemezi wao na uchumi wa nchi kwa kuwa hawataweza kulipa kodi stahiki.

Malalamiko ya wadau ni kukosekana kwa meza au kusikiliza madai yanayotolewa dhidi ya chombo husika kabla ya hukumu, au wakati mwingine hukumu kutoka bila kugusa utetezi wa waliotuhumiwa, na matokeo yake inaleta taswira mbaya kwa nchi katika uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa.

Pia wadau wa habari wana malalamiko dhidi ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na kanuni za utangazaji, hivyo tunaamini kwa kuwa chini ya waziri mmoja sasa changamoto nyingi zitatuliwa na kuondoa malalamiko.


Kwenye Wizara ya Nishati, Makamba, anakabiliwa na kibarua cha kuhakikisha wananchi wanaunganishiwa umeme hasa vijijini, kasi ya kubadili nguzo za mbao kwenda za zege, usambazaji wa gesi kwenye makazi ya watu na viwandani pamoja na kuhakikisha bei ya mafuta haizidi kupaa kwa sababu za ndani.

Kwa upande wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, kibarua ni kizito zaidi kwa kuwa kuna mradi mingi ya ujenzi ambayo inapaswa kukamilika ikiwamo reli ya kisasa na ianze kutumika kwa kadri ya muda wa mradi, ujenzi wa vivuko/ meli, ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato, Dodoma, madaraja na barabara za miji na majiji. Pia ununuzi wa meli kwenye maziwa.

Miradi hii yote inahitaji usimamizi wa karibu kwa kuwa inatumia mabilioni ya fedha, ambazo ni za Watanzania, lakini kukamilika kwake ni neema kwa kuwa huduma za usafiri zitakuwa rahisi na haraka, pamoja na maendeleo ya kiuchumi kwa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Mawaziri mlioteuliwa kaeni mguu sawa eeh

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko madogo ya mawaziri watatu watakaokuwa miongoni mwa askari wa miavuli anaotarajia wawe wachapakazi hodari kwenye uongozi wake.

Aidha, ameziba pengo la Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lililoachwa na Elias Kwandikwa, aliyefariki mwezi uliopita, kwa kumteua Dk. Stergomena Tax. Lakini pia, Jaji Eliezer Feleshi, ameteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mawaziri Profesa Makame Mbarawa wa Ujenzi na Uchukuzi, January Makamba wa Nishati na Dk. Ashatu Kijaji anayeongoza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndiyo waliokula kiapo mwanzoni mwa wiki hii kuanza majukumu mapya ya kiuongozi.

Wote watatu wamerudi kwenye kazi ambazo wamewahi kuzifanya siku za nyuma si wageni ila kwa Dk. Kijaji amepanda ngazi kwa vile awali alikuwa Naibu Waziri wa Fedha.

Wamekuwepo kwenye baraza la awamu ya tano na sasa wanaendelea kwenye ngwe ya kwanza ya miaka mitano ya uongozi wa Rais Samia.

Rais Samia kama alivyosema wakati wa kuwaapisha kuwa kwa miezi sita ya awali alikuwa anawatazama na anachotaka ni kuona adilifu, uaminifu na utiifu wao kwake na si kufanya vile mtu apendavyo.

Wakati huu kuna mijadala na mitizamo mingi kuhusu utendaji kazi, wananchi wakiangalia na kufuatilia mambo yanayoendelea.

Kwa mfano, shida ya maji ni kubwa majijini, mijini na vijijini. Watanzania wanaitazama Wizara ya Maji na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na kufuatilia hatua kwa hatua matatizo ya uhaba wa maji wanayoyaona yanaisha lini.

Si hivyo tu, umeme kukatika kila wakati na kwamba licha ya kuwa gharama za uunganishaji ni Shilingi 27,000 wateja wanaoomba umeme wanalalamikia unachelewa kuwafikia.

Licha ya Tanzania kuwa na barabara nzuri na za lami tatizo linalobakia ni lile lile serikali za mitaa kushindwa kuwekeza na kubadilisha uchumi wa maeneo ya wananchi zinapopita kwa kutumia utajiri wa barabara unaopita katika vijiji vyao.

Kwa mfano kutoka Arusha hadi Mbeya au Dar es Salaam hadi Arusha njiani kuna shughuli nyingi za uzalishaji na biashara, lakini sehemu kubwa ya maisha pembeni ya barabara hizo ni umaskini.

Tunaamini Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na wa TAMISEMI , Uwekezaji, Viwanda na Biashara watahamasisha ubunifu kwenye halmashauri ili kuanzisha shughuli za uwekezaji kando ya barabara kuu.

Kwa mfano kwa miaka 60 ya Uhuru eneo la Segera Tanga, limebakia kuuza machungwa na matunda mengine bila kuwa na viwanda na sehemu za kuhifadhi matunda hayo. Viongozi bungueni bonge mlete mabadiliko.

Macho na masikio ya Watanzania ni kuona na kusikia viongozi wanaofanyakazi na pengine kwa sababu Rais amesema kwenye uteuzi huo, ameweka koma na siyo nukta ni vyema wanaopewa wadhifa wa kuongoza nchi wakachapa kazi.

Wawe askari wa miavuli si kwa sababu watu wanatazama ni nani atabakia au ni yupi atakaondoka, bali wawe na moyo thabati wa kuleta maendeleo siyo kufurahia maisha wakati wapigakura wanateseka.

Rais ameshasema kuwa mchakato wa kuunda na kubadilisha baraza la mawaziri ni endelevu na kwa kwa kuwa CCM ina wabunge zaidi ya 350 wapigakura wanaamini kuwa hakuna sababu ya kuvumilia watendaji ambao hawatimizi malengo.

Rais anasema, wapo wengi wanaofanyakazi kwa uaminifu na wapo wengine ambao kama alivyosema kazi ya kubadilisha safu ya mawaziri ni endelevu huenda atawashughulikia kwa sababu hawamudu kazi zao.

Watanzania wanatamani kuona watu wanaofanyakazi kwa kasi ya kuboresha maisha ya watu na kuifanya Tanzania bora na mahali pazuri pakuishi.

Mawaziri wakumbuke kuwa watu wamechoka kuona shida ya maji, umeme kukatika kila wakati bila sababu za msingi, msongamano barabarani, uhaba wa dawa hospitalini wakati wanalipa kodi na tozo.

HABARI KITAIFA

## Machinga waomba kupangiwa maeneo yenye miundombinu

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAFANYABIASHARA maarufu kama machinga jijini hapa, wameiomba serikali kuwapanga katika maeneo rafiki ambayo yanafikika kwa urahisi.

Hayo yamejiri baada ya kauli ya Rais Samia aliyoitoa juzi kwa wakuu wa mikoa kuwapanga machinga kwa utaratibu maalum katika maeneo yao.

Wakizungumza na vyombo vya habari baadhi ya machinga waliomba kuendelea kubaki katikati ya jiji kwa sababu ya urahisi wa upatikanaji wa wateja.

Mfanyabiashara mdogo Anthony Joseph, alisema maeneo rasmi kwa ajili yao yapo nje ya mji na hayafikiki kwa urahisi na pia katikati ya mji ni rahisi kupata wateja wanaotoka nje ya mkoa.

Alisema bidhaa zao wamepanga vizuri pembezoni mwa barabara na watembea kwa miguu wanapita vizuri pamoja na vyombo vya moto.

Majid Luizer alisema mpangilio wa machinga sio mzuri kutokana na msongamano ikiwamo vyombo vya moto kupita kwa shida pamoja na watembea kwa miguu na kumpongeza Rais kwa tamko lake.

Aliiomba serikali kuwahamisha machinga kutoka maeneo ya barabarani kwa kuwa inaweza kuhatarisha maisha yao endapo ajali itatokea.

Zuwena Ramadhani alisema endapo watapangwa vizuri katika maeneo yao vyombo vya usafiri vitapita kwa urahisi pamoja na waenda kwa miguu.

Pia, mfanyabiashara mkubwa Steven Joseph, alimpongeza Rais kwa kauli yake kwa kuwa machinga wameweka msongamano katika maeneo wanayofanyia biashara na endapo tamko hilo litatekelezwa itasaidia kupunguza msongamano.

Alisema maeneo mengine waliyopanga machinga mbele ya wafanyabiashara wakubwa ni kwa ajili ya maegesho ya magari na wateja wao wanapata ugumu wa kununua bidhaa na kupakia kwa urahisi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa machinga Wilaya ya Nyamagana, Matandua Ramadhani, alisema wanaunga mkono tamko la Rais na kwamba machinga wapo maeneo yasiyo rasmi kutokana na kupisha ujenzi wa soko unaoendelea.

Alisema wafanyabiashara wengi waliopo katika maeneo hayo wanasubiri ujenzi huo ukamilike wahamishe biashara zao kutoka maeneo hayo.

"Tunaiomba serikali itujengee maeneo mengine rafiki tofauti na nje ya jiji ambayo yatakuwa rafiki na pia tunaomba tusitafsiriwe vibaya kwani biashara zetu tunategemea kufanya maeneo yanayofikiwa kwa urahisi na wateja wanaozunguka katikati ya jiji," alisema Ramadhani.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kivulini, Yasin Ally, alimpongeza Rais kwa maelekezo aliyoyatoa na kwamba shirika lao lilifanya utafiti katika Halmashauri za Nyamagana na Ilemela na kubaini uholela katika sekta hiyo, uhaba wa miundombinu rafiki na wezeshi pamoja na machinga kutokuwa na kazi ya kudumu.

Alisema utafiti huo ulibaini asilimia 60 ya machinga ni wanawake na wamejenga masoko yenye mazingira rafiki kwa kuwa na maeneo maalum ya maelezi kwa watoto, gharama nafuu pamoja na kuwa na mfumo wa kanzi data kwa ajili ya kuwatambua machinga na biashara zao.

# Utafiti wa HakiElimu wabaini uhitaji mtaala wenye ulemavu

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya HakiElimu imezindua matokeo ya utafiti wa upatikanaji wa elimu jumuishi ya awali kwa watoto wenye ulemavu huku ikionyesha kuwa bado mtaala na muhtasari wa elimu ya awali na miongozo inahitaji kuboreshwa na kusisitiza utoaji wa elimu hiyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ripoti hiyo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalaghe, alisema baadhi ya sababu zinazozuia upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu ni unyanyapaa,wazazi kusita kuwaandikisha shule na kuwaficha nyumbani.

Sababu nyingine ambayo alisema imebainika kuwa kikwazo kwa kundi hilo la watoto kushindwa kupata elimu hiyo ya awali ni umbali wa kutembea kwenda shuleni na kushiriki kwenye shughuli za kijamii, ukosefu wa bajeti maalum ya serikali kwa ajili ya kundi hilo, uhaba wa wafanyakazi wenye mafunzo ya elimu maalum na ukosefu wa vifaa stahiki vya kujifunzia na kufundishia.

"Utafiti unaonyesha kuwa hali ya uandikishaji kwenye ngazi ya elimu ya awali inabadilika, uandikishwaji wa watoto wenye ulemavu wa viungo na afya ya akili inaongoza kwa miaka yote ikilinganishwa na ulemavu wa kuona ambao ulikuwa wa chini zaidi ,"alisema Dk. Kalaghe.

HakiElimu ilipendekeza kwamba kuna haja kwa serikali kupitia upya mitaala na mihutasari ya elimu ya awali ili kuboresha vipengele vya mitaala vinavyohusiana na viashiria vya ufanisi wa utendaji wa watoto wenye ulemavu wa kuona na viziwi.

Mapendekezo mengine ya taasisi hiyo ni kwa serikali kuongeza bajeti na matumizi ya fedha kwenye kuboresha elimu jumuishi ya awali pamoja na kuharakisha utekelezaji wa rasimu ya fomula ya ruzuku ya wanafunzi ambayo pia inalenga watoto wenye mahitaji maalum shuleni.

"Serikali iandae mwongozo wa lugha nyepesi kwa ajili ya wadau wote wakiwamo walimu wa madarasa ya awali, kuwatambua watoto wenye uoni hafifu, viziwi na wenye ulemavu wa akili wakati wa kuwaandikisha shule, iandae miongozo na vigezo vya viwango vya chini vinavyotakiwa kuwapo kwenye madarasa ya awali ili kuwasaidia na kuwaongoza walimu kufanya madarasa yao yawe jumuishi zaidi," alisema Kalaghe .

"Serikali pamoja na wadau ianzishe vituo shikizi ambavyo vitatoa fursa kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali kwenye shule zilizo karibu na ndani ya jamii zao, iboreshe mfumo wa ukusanyaji takwimu kwa kundi hilo kwa kuzingatia umri, aina ya ulemavu na jinsi."

Pia, HakiElimu ilipendekeza Taasisi ya Elimu Tanzania kufanyia maboresho ya vitabu vya elimu ya awali na vya hadithi ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu wa kuona.



Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC) ambalo ni tawi la Benki ya Dunia, Frank Ajilore (kushoto), akipokea kitabu kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi, alipotembelea makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. Ziara hiyo ilijikita katika kuboresha ushirikiano wa taasisi hizo mbili na namna ya kuimarisha huduma za kifedha kwa wanawake nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka zavalia njuga upotevu maji

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MAMLAKA za Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro, Dodoma na Singida zimeanzisha kampeni ya kutokomeza upotevu wa maji ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo bila matatizo na kwa bei nafuu. Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), Mhandisi Tamimu Katakweba, alisema kuwa kitendo cha kupambana na upotevu wa maji ni hazina kwa taifa.

"Kumekuwa na upotevu wa maji unaofanyika kwa njia mbalimbali ikiwamo wizi wa maji na mvujo, hivyo kusababisha mamlaka za maji kupata hasara. Tumeamua kukabiliana na tatizo hili," alisema.

Katakweba alisema kitendo cha mvujo wa maji husababisha baadhi ya watu kutopata huduma ya maji ya uhakika lakini pia yanapokuwa yakipatikana huwa na gharama kubwa kitendo ambacho kimekuwa kikisababisha kero kwa wananchi.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Maji imeziagiza mamlaka za maji kuhakikisha kero zote za maji zinatatuliwa ili wananchi waondokane nazo jambo litakalosaidia kuwatua wanawake ndoo za maji kichwani.

Mhandisi Katakweba pia aliwataka wananchi wote kuwa walinzi dhidi ya wanaohujumu miundombinu ya maji kwa kutoa taarifa kwa mamlaka za maji ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa kwa wote wakaobainika kuhusika na hilo.

Katakweba aliwataka watumishi wa mamlaka za maji katika mikoa hiyo kuwa wazalendo kwa taifa lao na kuepuka kuwabambikia wateja bili za maji, kuepuka rushwa pamoja na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yote hatari.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sindiga, James Malima, alisema utopevu wa maji ni adui mkubwa kwa mamlaka hizo, hivyo wameamua kukabiliana na tatizo hilo.

Malima aliwataka wasoma mita wote wa mamlaka hizo za Morogoro, Dodoma na Singida kuacha tabia ya kuwabambikia bili wateja kwa kuwa kitendo hicho hakileti picha nzuri kwa mamlaka.

Alex Mpagama, Meneja Biashara wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) alishukuru ushirikiano wa Wizara ya Maji na kusema kampeni hiyo itasaidia kupunguza tatizo la upotevu wa maji.

HABARI KITAIFA

# Ukatili kwa wanawake, watoto waiamsha LHRC

**Na Thobias Mwanakatwe**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimesema matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini yaliyoripotiwa polisi yameongezeka.

Kimesema yameongezeka kutoka 23,685 mwaka 2019 hadi kufikia 26,544 mwaka jana sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari akitangaza kuzinduliwa kwa mbio maalum zitakazojulikana kama Haki Marathon ukiwa ni mkakati wa kuwawezesha Watanzania kutambua wajibu wao wa kulinda haki za binadamu nchini.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020, matukio 36,940 yalifikishwa vituo vya polisi kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019 ikiwa ni sawa na matukio 7,388 kwa mwaka.

Alisema kutokana na ukatili huo kuongezeka, LHRC imeamua kuanzisha mbio hizo ambazo zinatarajia kushirikisha watu zaidi ya 1,000 kutoka ndani na nje ya nchi ambazo zitakuwa zikifanyika kwa njia ya mtandao kuanzia Oktoba 17 na kufikia kilele 10 Desemba 2021.

"Kuanzishwa kwa Haki Marathon ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo Kauli mbiu ya Haki Marathon ni 'Haki ni Maendeleo," alisema.

Henga alisema wazo la kufanya marathon kwa njia ya mtandao limekuja kama sehemu ya mkakati wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wa kujenga uelewa na kuwawezesha Watanzania kutambua wajibu wao wa kulinda haki za binadamu nchini.

" Janga linaloendelea la UVIKO 19 limelazimisha Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuratibu marathoni kwa njia tofauti kwa kuzingatia miongozo ya kiafya inahohimiza kuepuka misongamano mikubwa," alisema.

Alisema mbio hizi zitatoa fursa kwa mtu yeyote kushiriki ili mradi tu awe amejisajili na kulipia ambapo zitadumu kwa muda wa wiki saba na watu kutoka maeneo tofauti ya nchi na hata walioko nje ya mipaka ya nchi wanaweza kushiriki kwa kasi watakayochagua na kwa wakati watakaochagua wenyewe.

Henga alisema baada ya kumaliza mbio, washiriki kutegemeana na eneo lake ataelekezwa wapi na wakati gani wa kwenda kupokea medali zao.

"Haki Marathon itakuwa na makundi matatu ya mbio ambayo ni Kilometa 21, Kilometa 10 na kilometa 5. Wote watakaokamilisha mbio walizochagua watapewa medali," alisema.

Aliongeza kuwa mbio za Haki Marathon zinalenga kutafakarisha umma wa Watanzania juu ya jukumu la kila mmoja kulinda na kuheshimu haki za binadamu hasa tunapojiandaa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo itaadhimishwa ulimwenguni kote Desemba 10, 2021.




Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Watu wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga (wapili kulia), akikata utepe kuzindua ugawaji wa pikipiki 65 iliyoandaliwa na NACOPHA kupitia mradi wa Hebu Tuyajenge, unaowezeshwa na Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), jijini Dodoma, kwa ajili ya kutumika katika utekelezaji wa mradi huo kwenye halmashauri 65 za mikoa 22 ya Tanzania Bara. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NACOPHA Tanzania, Deogratius Rutatwa na (kulia) ni Samweli William kutoka Mtandao wa Vijana wanaoishi na VVU Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Afariki dunia ajali ya trekta na Hiace

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTU mmoja ambaye hajafahamika jina wala makazi yake, amefariki dunia na wengine saba kujeruhiwa, katika ajali ya gari na trekta, iliyotokea Kijiji cha Ishinabulandi, wilayani Shinyanga.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari na kwamba tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 4:30 usiku.

Alisema gari hiyo aina ya Hiace yenye namba za usajili T470 DEL, ilitokea wilayani Kahama kwenda Shinyanga mjini na ilipofika katika kijiji hicho iligongana na trekta lenye namba za usajili T 623 CKY na kusababisha kifo cha abiria mmoja huku watu saba wakijeruhiwa.

*Watu saba waliojeruhiwa katika ajali hii ni pamoja na Shija Deus, Mohamed Juma, Venance John, Maneno Charles, Paulo Stephano, Shabani Mohamed na Josia Magabe, wote wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga," alisema Kyando.

Alisema chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa Hiace, Sudi Ntawigaya kutaka kuyapita magari mengine akiwa mwendo kasi na kisha kuligonga trekta hilo lililokuwa likiendeshwa na Shija Steven.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka dereva wa Hiace, ambaye alikimbia baada ya kusababisha ajali hiyo.

Kamanda huyo alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto mkoani Shinyanga kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali.

**Watu saba waliojeruhiwa katika ajali hii ni pamoja na Shija Deus, Mohamed Juma, Venance John, Maneno Charles, Paulo Stephano, Shabani Mohamed na Josia Magabe, wote wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga.**

# RC ataka wazee kuingizwa mfumo matibabu bure

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, ameziagiza halmashauri za mkoa huo kuhakikisha zinawaingiza wazee wote wanaostahili kwenye mfumo wa matibabu bure na kupewa vitambulisho vyao vya uzee kabla ya mwisho wa Oktoba.

Rubirya alitoa agizo hilo juzi wakati akizindua Baraza la Wazee wa Mkoa wa Njombe uliofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, mjini hapa.

"Naziagiza halmashauri zote sita kuhakikisha wazee wote wanaostahili wanaingizwa kwenye mfumo wa matibabu bure na wanapewa vitambulisho vyao kabla ya mwisho wa Oktoba, mwaka huu. Ninawaagiza wakurugenzi wote kuhakikisha wanasimamia hili," alisema Rubirya.

Aidha, mkuu huyo wa mkoa alisema mpaka sasa wazee 13,100 pekee wasio na uwezo ndio waliopatiwa vitambulisho vya uzee.

"Nimefahamishwa kuwa hadi sasa ni wazee 13,100 wasiokuwa na uwezo kati ya wazee 39,700 waliotambuliwa na wamepata vitambulisho hivyo vinavyowawezesha kupata matibabu bure," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wazee, Mwenyekiti wa Baraza hilo Mkoa wa Njombe, Papius Mvunyi, alimshukuru mkuu wa mkoa kwa kutoa agizo hilo huku akisisitiza vitambulisho hivyo kwenda sambamba na utoaji wa huduma za afya bora kwa wazee.

"Nimshukuru mkuu wa mkoa kwa maagizo aliyoyatoa hasa kwa wazee kupata vitambulisho vile ingawa kiuhalisia wengi wanalalamika vile vitambulisho havizingatiwi. Nitawaomba wazee kutambua wanaokiuka na kuwafikisha mahali husika kwa kuwa sasa serikali inatuona," alisema Mvunyi.

# Waandishi wanolewa habari za UVIKO-19

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuandika habari zilizothibitishwa na wataalamu wa afya ambazo zinahusiana na chanjo ya UVIKO-19 ili kuepuka upotoshaji katika jamii.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, katika mkutano wa kimtandao kwa vyombo vya habari na AZAKI nchini.

Dk. Subi alisema ugonjwa wa corona bado upo, lakini baada ya watu zaidi 340,000 kupata chanjo ambazo ni salama maambukizi nchini yamepungua.

Aliwataka waandishi kutoandika habari za upotoshaji na kupunguza matumizi ya mitandao yasiyo na tija badala yake wawe mabalozi wa uhamasishaji.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kutafuta rasilimali nyingi ikiwamo fedha ili kupambana na ugonjwa huo na kuhakikisha chanjo hizo zinapatikana katika mikoa yote.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya ikiwamo kuvaa barakoa ili kupambana na kirusi hicho.

Akizungumzia umuhimu wa chanjo ya Covid - 19, Profesa Harun Nyagori, ambaye ni daktari bingwa mwandamizi wa magonjwa ya ndani na moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwetwe (JKCI), alisema chanjo ya UVIKO-19 ni salama na haina madhara yoyote kwenye mifumo ya uzazi wala haisababishi kuganda kwa damu kama inavyoelezwa.

Profesa Nyagori alisema utafiti uliofanywa hauonyeshi mtu atakayepatiwa chanjo ya UVIKO 19 atapata tatizo la uzazi na badala yake ilionekana kuna wanaume walipungukiwa nguvu za kiume baada kukutwa na UVIKO 19.

Alisema kitu chochote kipya kwenye afya kinapoletwa lazima kiwekewe utaratibu wa ufuatiliaji ikiwamo kujaza fomu ya ridhaa (consent form) ambayo kwenye matibabu ni jambo la kawaida.

"Mfano kwenye upasuaji lazima ujaze consent form ndiyo ufanyiwe upasuaji pia hivi karibuni kuanzia mwaka 2018 hadi 2020 wajawazito wenye maambukizi ya HIV walikuwa wanajaza fomu hiyo ili waweze kupewa dawa za ARV iitwayo doluteghavir," alisema.

Aliogeza kuwa hata suala la ujazaji wa fomu kwenye chanjo ya UVIKO-19 ni muhimu na ufuatiliaji ukikamilika hiyo fomu haitajazwa tena na kwamba watu watakiwa kupata chanjo chanjo bila kujaza fomu.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Freedom House Daniel, Lema, aliishukuru Wizara ya Afya kwa kutoa wataalamu ambao watatoa majibu ya maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa na jamii juu ya chanjo ya UVIKO-19.

Lema aliwataka wataalamu kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kutoruhusu uvumi wa taarifa zisizo na ukweli kutoka kwa watu wenye lengo baya la kupotosha ukweli.

Aidha, aliahidi kuendeleza ushirikiano wa kufanya kazi na MPC na wizara ili kutekeleza mapambano dhidi ya UVIKO-19.

# Jaji ataja viashiria uchaguzi huru, usio na malalamiko

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

JAJI mstaafu wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Mbarouk Salim Mbarouk, amesema uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali za kufuatwa, ambazo zinaweka msingi imara wa uchaguzi wenye uwazi na usio na malalamiko au vurugu.

Aliyasema hayo mjini Chakechake alipokuwa akifungua mafunzo kwa watendaji wa wasimamizi wa uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde.

Aliwataka wasimamizi hao kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), huku wakiepuka kufanya kazi kwa mazoea ili kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika katika hali ya amani na utulivu.

Aliwasihi watendaji hao wahakikisha wanawashirikisha wadau wote wa uchaguzi wakiwamo wanasiasa ili kuwe na uchaguzi huru na wa haki.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi NEC, Hamidu Mwangu, aliwataka watendaji hao kuwa makini katika kufuata maelekezo watakayopewa na NEC katika kutekeleza majukumu hayo kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa.

Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde Wilaya ya Micheweni mkoa wa Kaskazini Pemba ambao unatarajia kufanyika Oktoba 9, mwaka huu, kufuatia kujiuzulu kwa mbunge mteule wa jimbo hilo, Sheha Mpemba Faki, ambaye alitangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi mdogo uliofanyika Julai 18, mwaka huu kufuatia jimbo hilo kuwa wazi baada ya kufariki dunia kwa aliyekuwa mbunge wajimbo hilo, Khatib Said Haji (ACT) Mei 20, mwaka huu.

Faki (CCM), alijiuzulu baada ya uchaguzi huo mdogo kukumbwa na malalamiko kutoka Chama cha ACT-Wazalendo.



Katibu wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA) Kanda ya Kaskazini, Godwin Mpinga (mwenye koti), akitoa elimu kwa abiria ndani ya basi, jijini Arusha mwishoni mwa wiki, kuhusu jinsi ya kujua haki zao na namna ya kujikinga na ugonjwa wa corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wenye ulemavu akili na viungo waombewa bajeti

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeombwa kutenga bajeti ya kutoa ruzuku maalum kwa ajili ya kuvisaidia vituo vya kulea watoto wenye ulemavu wa afya ya akili na viungo.

Lengo la fedha hizo ni kukidhi mahitaji yao muhimu wanayoyakosa.

Mwanaharakati wa haki za watoto wenye ulemavu, ambaye ni mwasisi wa kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu wa akili na viungo cha EMFERD, Josephine Bakhita, alisema hayo jana na kwamba mahitaji ya msingi ya watoto wenye ulemavu wa akili na viungo ni muhimu kuwapo kwa wakati wote.

Bakhita alisema watoto hao wana mahitaji mengi ya msingi ambayo vituo vingi vya kuwalea hawezi kumudu ambayo ni kuwapatia watoto chakula, matibabu, elimu na mazoezi ya kuimarisha viungo vyao.

Hivyo alisema serikali inapaswa kutupia jicho kwenye vituo hivyo kwa kuvipatia ruzuku, ambayo itavisaidia na kuepukana na baadhi ya watoto kukosa vitu muhimu ikiwamo elimu na mazoezi ya viungo.

"Naiomba serikali, itupie jicho la huruma vituo vya kulelea watoto wenye ulemavu wa akili na viungo kwa kuwa licha ya kwamba watoto hao wana mahitaji mengi wamekuwa wakiyakosa," alisema.

Aidha, alisema serikali ikiwa makini katika hilo, itasaidia watoto hao kwa umakini zaidi kwa sababu kwa sasa mwamko wa jamii kuwasaidia watoto hao sio mkubwa.

Naye Ofisa Habari na Uhusiano wa Taasisi hiyo, Victor Makinda, alishauri serikali kuona haja ya kusaidia vituo vya kulelea watoto wenye ulemavu wa viungo na akili kwani bado suala la kuwaficha watoto majumbani lipo hasa kwenye maeneo ya vijijini.

# Kamati kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji

**Na Mbaraka Kambona,** KILWA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka viongozi wa serikali kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, kata na wilaya kuunda kamati za maridhiano kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikijitokeza katika baadhi ya maeneo na kuleta madhara kwa jamii.

Ulega alitoa agizo hilo kwenye ziara aliyoifanya Kijiji cha Nakiu, wilayani Kilwa, mkoani Lindi Septemba 13, 2021 baada ya kupokea kero zilizohusu migogoro mingi iliyoanza kujitokeza katika wilaya hiyo inayowahusisha wakulima na wafugaji.

Katika mkutano huo wananchi wa kijiji hicho walililalamikia Jeshi la Polisi kutochukua hatua za haraka wanapopelekewa taarifa za wafugaji wanaolisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Walisema wafugaji wanaofanya vitendo hivyo wengi ni wahamiaji katika maeneo hayo na wanasababisha matatizo makubwa ikiwamo kuharibiwa kwa mazao yao na wanapotaka kulinda mazao yao wanaishia kupata kipigo.

Kufuatia malalamiko hayo, Waziri Ulega alitoa maelekezo kwa watendaji wa serikali kuanzia ngazi za chini kuanzisha kamati za usuluhishi ili ziwe zinashughulika na migogoro hiyo mapema kabla haijakuwa mikubwa na kuleta madhara.

Aliongeza pia kwa kulitaka Jeshi la Polisi wilayani humo kuhakikisha wanatenda haki kwa kila mtu na kwa usawa ili kuondoa lawama zinazowakabili za kuonekana wanawapendelea wafugaji kuliko wakulima.

Vilevile, aliwaelekeza watendaji wilayani humo kuwa katika kamati watakazoziunda waandae mpango mzuri wa kuweka njia kwa ajili ya kupitishia mifugo ili isiwe inapita katika mashamba ya wakulima.

Waziri Ulega pia kukemea vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vinavyofanywa na wakulima pamoja na wafugaji akisema kuwa kufanya hivyo ni kosa na ni miongoni mwa vitendo vinavyochangia uvunjifu wa amani.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa, katika kuhakikisha maelekezo hayo ya Naibu Waziri yanafanyiwa kazi kwa haraka aliwaagiza watendaji wake kuhakikisha kamati hizo zinaundwa ndani ya wiki moja.

Kuhusu suala la kuweka njia za mifugo, Kawawa alitoa mwezi mmoja kwa wataalamu wa mifugo kwa kushirikiana na wafugaji na wakulima kuhakikisha njia hizo zinawekwa ili kupunguza usumbufu wa mifugo katika mashamba ya wakulima.

Mkuu wa Wilaya pia aliwataka wafugaji kuchimba mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo na kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza migogoro ya mara kwa mara na wakulima.

Kabla ya ziara hiyo ya Waziri Ulega wilayani humo, siku chache zilizopita wafugaji waliuawa kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji katika Kijiji cha Nanjilinji.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa tatu kushoto), akizungumza na kikosi kazi cha kusafisha mito alipotembelea kukagua Mto Mbezi, eneo la Kimara B, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TGNP yampa kongole Rais Samia kwa uteuzi wa wanawake nafasi nyeti

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BODI ya Wakurugenzi na Wafanyakazi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuzingatia jinsia katika uteuzi wa nafasi mbalimbali za uongozi.

Pongezi hizo zimetokana na uteuzi wa mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliofanyika tarehe 12 Septemba, mwaka huu, ikiwa mwelekeo wa kufikia malengo ya asilimia 50 kwa 50 ya uteuzi wa mawaziri.

Akizungumza kwa niaba ya bodi hiyo jana mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema katika uteuzi huo, Rais aliteua viongozi watano, mawaziri wanne wakiwamo wanawake wawili, hivyo kufikia asilimia 50/50 ya uteuzi huo wa mawaziri.

Pia Rais alimteua Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Elieza Feleshi, ambaye ni mwanamume. Katika uteuzi huo, Dk. Stergomana Tax aliteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza wizara hiyo tangu uhuru. Pia alimteua Dk. Ashatu Kijaji kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Sambamba na wanawake hao, January Makamba aliteuliwa kuwa Waziri wa Nishati na Prof. Makame Mbarawa Mnyaa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Kwa ujumla, katika uteuzi huo, Rais aliteua wanawake wawili sawa na asilimia 40 na wanaume watatu sawa na asilimia 60.

Alisema mbali na kuzingatia idadi ya wanawake katika uteuzi huo, TGNP inatambua jitihada za Rais katika kuhakikisha wanawake wanashika nafasi muhimu kwa mustakabali wa nchi, nafasi ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikishikwa na wanaume.

Pia alisema katika uteuzi huo, Tanzania imetengeneza historia kwa Dk. Tax kuwa mwanamke wa tatu kuwa Waziri wa Ulinzi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki akiungana na Raychelle Omamo wa Kenya (Mei, 2013- Januari, 2020) na Monica Juma (Jan, 2020 hadi sasa).

Alisema kwa ujumla, uteuzi huo umeongeza nafasi za wanawake mawaziri kufikia saba sawa na asilimia 30.4 kutoka watano waliokuwapo, sawa na asilimia 21.7 wakati huo wanaume wakiwa ni 16 sawa na asilimia 69.6 kutoka 18 sawa na asilimia 78.2 Machi, mwaka huu alipochukua madaraka ya urais akichukua nafasi ya hayati Rais John Magufuli.

Kutokana na hatua hiyo, Liundi alitoa wito kwa viongozi wanawake na wanaume walioteuliwa na Rais kutumia nafasi na taaluma zao vyema kumsaidia Rais kutimiza majukumu yake ya kuleta maendeleo endelevu na jumuishi nchini.

# Wanaochimba mchanga bila vibali waonywa

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewaonya watu wanaovamia mito na mabonde na kuchimba mchanga bila kuwa na vibali kwamba atakayekamatwa atakuwa mfano kwa wengine.

Alitoa onyo hilo wakati wa majumuisho ya ziara yake kukagua mito na mabonde mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam kuangalia kazi iliyofanywa na kikosi kazi kinachofanyakazi ya kudhibiti mmomonyoko kwenye mito akiwa eneo la Ulongoni.

Kikosi kazi hicho kinawahusisha maofisa wa polisi, Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA), Mkoa wa Dar es Salaam, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na maofisa kutoka manispaa za Dar es Salaam.

Jafo alisema serikali inatumia gharama kubwa kutengeneza kingo za mito kuhakikisha watu walioijirani na mabonde hayo wanakuwa salama hivyo kuendelea kuchimba mchanga ni kuhatarisha maisha ya watu.

Alisema kumekuwa na changamoto kubwa ya kutunza mito na mafuriko yamekuwa yakitokea na sababu kubwa ikiwa ni uchimbaji wa mchanga kwenye maeneo hayo.

"Watu wote wanaovamia mito na kuchimba mchanga bila vibali na kusababisha mmomonyoko na kuhatarisha maisha ya watu na watakaokiuka agizo langu watachukuliwa hatua kali sana itakuwa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo," alisema.

Alisema wizara yake iliunda kikosi kazi maalum kusimamia usafishaji wa mito na alikipongeza sana kikosi kazi hicho kwa kazi kubwa iliyofanyika kwani kimefanikiwa kusafisha mito hiyo kwa urefu wa kilomita 47.

Alisema atahakikisha kikosi kazi hicho kinawezeshwa kifedha ili kuhakikisha kazi nzuri waliyoifanya inaendelea kwenye mikoa mbalimbali nchini huku akisema kuwa lazima wananchi waheshimu sheria za nchi na kuachana na uvamizi wa mito na mabonde.

Alisema serikali imeifanya ajenda ya mazingira kuwa ni endelevu hivyo kila Mtanzania anapaswa kuwa mlinzi wa mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo kwani serikali inatumia gharama kubwa kutengeneza miundombinu inapoharibiwa.

Angela Kibiriti, mjumbe wa kikosi kazi hicho akitokea Jeshi la Polisi, alisema kikosi kazi hicho kimefanikiwa kutoa elimu ya athari za kukaa jirani na mito na kuwa walinzi wa watu wanaochimba mchanga.




Ukurasa 12

Mabadiliko barazani wengi wanaposaka, kuibua vyanzo



Ukurasa 13

Mama Stergomena Tax maarufu kuvunja miiko



Ukurasa 14

ALPHA CONDE

**Alijidai hayupo anayetosha kuiongoza Guinea**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 15, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


KUTOKA LIUNDI HADI MUTUNGI

# Kinachowatofautisha wasajili vyama vya siasa nchini ni hiki

• Baadhi ya wadau washauri Ofisi ya Msajili ifutwe

**Na Sabato Kasika**

UNAPOIZUNGUMZIA Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, moja kwa moja unagusa eneo la sheria za nchi, kazi iliyoanza pale Tanzania ilipolazimika kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Uwapo wa vyama vingi, uliisukuma nchi kuunda Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ambayo pamoja na majukumu mengine, inawajibika kusimamia Sheria ya Vyama vya Siasa. Kwa kusimamia Sheria hiyo Na. 5 Mwaka 1992 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010, ofisi hiyo inatakiwa kuhakikisha uwapo na ukuaji wa demokrasia ya vyama vingi nchini kwa maendeleo ya taifa.

Taasisi hiyo hadi sasa imeongozwa na wasajili watatu -- wa kwanza akiwa ni George Liundi aliyeshika nafasi hiyo kuanzia mwaka 1992 hadi 2001, akifuatiwa na John Tendwa aliyeongoza hadi mwaka 2013 alipokabidhi kiti kwa bosi wa sasa, Jaji Francis Mutungi.

Kuanzia msajili wa kwanza hadi wa sasa, kila mmoja kwa wakati wake alitimiza wajibu wake na sasa jukumu hilo analo msajili aliyepo Jaji Mutungi, ambaye naye anaendelea kutimiza wajibu wake. Mchambuzi wa Siasa na Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anaoiona Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kama imekaa vibaya na kwa mtazamo wake ni vyema isiwapo.

"Kwa nchi zingine huko duniani, vyama vya siasa vinasajiliwa na serikali na kuendesha shughuli zake na hakuna kiranja au ofisi inayoitwa ya Msajili wa Vyama vya Siasa kama ilivyo hapa nchini," anasema Mwakagenda.

Anafafanua kuwa vyama vya siasa ni serikali inayongojea kushika uongozi wa nchi, hivyo vinapaswa kuachwa viendeshe shughuli zake za kisiasa kuliko ilivyo sasa.



Jaji Francis Mutungi.

Kwa hali ilivyo nchini kwa sasa, mchambuzi huyo anaona ndicho kiini cha malalamiko kutoka kwa vyama hivyo yaliyojikita katika madai ya kudhibitiwa.

"Nizungumzie wasajili wa vyama, ni kwamba, alipoingia Liundi, tulikuwa tunashangaashangaa, kwani ilikuwa ni mara ya kwanza kuingia kwenye mfumo huo ingawa ulikuwapo miaka ya 60," anasema.

Anaongeza kuwa hata awamu ya Tendwa Watanzania walikuwa hawajachangamka zaidi na mwamko wao kwenye siasa za vyama vingine mbali na CCM umekuja huku sheria ya vyama ikiwa imebadilishwa.



John Tendwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

"Kwa ujumla ni kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatakiwa kuwa mwezeshaji na mlezi wa vyama hivyo vistawi, lakini inapokuwa kinyume, haina afya kwa taifa," anashauri Mwakagenda.

Mchambuzi huyo ana maoni na ushauri kwa wadau, ambao wamekuwa wakidai Katiba Mpya, wasisahau kuomba Ofisi ya Msajili wa Vyama ifumuliwe, ili kulea vyama na kuviwezesha kujitanua katika jamii.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anaona kwa sasa vyama vya upinzani viko hoi na vinahitaji kusimamiwa, ili viwe na nguvu mpya.

"Watu hawaoni kwa nini wagombee uongozi kupitia upinzani, wanajua watashindwa tu, kwa sababu ya kubanwa, pia wanasiasa wanakuwa na upinzani wenye chuki, ambao kimsingi si siasa zenye tija," anahadharisha.

Kiongozi huyo anamshauri Msajili kuliona hilo na kulifanyia kazi, ili watu wawe wanapingana kwa hoja na sio kuwa na siasa za kuchukiana na visasi.

"Ninakumbuka wakati wa kutafuta maoni ya kurejesha vyama vingi vya siasa, asilimia 20 ya Watanzania walitaka nchi iwe na vyama hivyo, lakini Mwalimu Julius Nyerere akashauri maoni ya wachache yakubaliwe," anasema Ngawaiya.

Anaongeza kuwa baada ya vyama vingi kuruhusiwa, Liundi alivilea vikakua na kufanikiwa kupata wabunge na madiwani

INAENDELEA UK.12

# Mabadiliko barazani wengi wanaposaka, kuibua vyanzo

**Na Nimi Mweta**

MIGONGANO ya mawazo imeshamiri maeneo tofauti, kuanzia mitandaoni, mazungumzo ya vyombo vya habari au vijiweni mitaani, kuhusu vyanzo vya mabadiliko, ambayo si madogo na si makubwa katika Baraza la Mawaziri yaliyoshuhudiwa jana.

Rais Samia Suluhu Hassan mwisho wa wiki iliyopita aliteua mawaziri wanne na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuondoa waliokuwapo, isipokuwa kwa nafasi ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo ilikuwa wazi kutokana na kifo cha Elias Kwandikwa. Rais anaweka historia kwa kumteua mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo; akihutubia baada ya kuwaapisha alitaja sababu.

Kwa maana hiyo uteuzi unaong'ara zaidi ni wa Dk Stergomena Tax, katika nafasi hiyo nyeti, na Rais Samia anaeleza kuwa akiwa katika nafasi ya Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Ushirikiano Kusini mwa Afrika (SADC), mtawala huyo na mwanadiplomasia aliongoza shughuli za ushirikiano wa usalama eneo hili. Anataja kuwa Tanzania ina askari wanaosaidia kulinda amani na kupambana na ugaidi nchini Msumbiji na kurudisha amani eneo la mashariki la DRC, hivyo anaelewa vyema masuala mbalimbali ya ushirikiano na mahitaji ya wapiganaji walioko huko. Anaeleza matazamio kuwa msaada wa mkuu wa majeshi kufanikisha hilo na kwa maana hiyo uteuzi wake haukuwa tu wa kuvunja mwiko wa waziri mwanamke.

Penginepo vyanzo vya kubadilishwa mawaziri vilikuwa wazi ukiangalia mtiririko wa habari, ila kutokana na yaliyopita mwanzoni, wanaopewa nafasi hizo, ambao kimsingi wanarudi katika Baraza la Mawaziri na siyo wateuliwa wapya zimeleta minong'ono kadhaa. Labda anayebishaniwa zaidi ni January Makamba, mbunge wa Bumbuli, ambaye amewahi kushika nyadhifa tofauti kama Naibu Waziri na Waziri awamu ya nne, na mapema awamu ya tano. Ila maelezo yaliyotolewa na wakuu wa nchi katika hafla hiyo kwa jumla yalitosheleza, hasa kuwa awali aliongoza Kamati ya Bunge inayoshughulia masuala ya nishati; anayajua. Kwa maana hiyo kamati za bunge zinakuwa ni kituo cha kutayarisha wabunge kuwa mawaziri pale nafasi inapotokea, ingawa si rahisi kukumbuka ni lini ilielezwa kuwa aliyeteuliwa nafasi hii au ile aliwahi kuongoza kamati husika bungeni.



Mkitongoji Said Malenga, pamoja na siasa, ni mkulima wa matunda anayehamasisha kilimo hai. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> Mengine ni mapito tu, ila Rais Samia amedhihirisha kumwamini pia.

Lakini hata bila kutajwa waziwazi ni lazima hali kama hiyo ichangie kupata anayefaa kuteuliwa, nje ya wazo kuwa wakuu wa nchi wanaangalia zaidi mahusiano au hasa kusukumiwa watu na waliowatangulia ni lazima watu waelewe kuwa uteuzi wa waziri ni jambo nyeti kwa Rais, kama ilivyokuwa kupata chanjo, kuwa huwezi kuliendea, bila kujiridhisha katika maeneo tofauti.

Wateuliwa wengine hawakuleta mjadala wa haraka, labda katika maeneo tofauti iwe ni ya kijamii au kisiasa, kwa mfano Dk Ashatu Kijaji amewahi kuwa Naibu Waziri Hazina, wakati Dk Eliezer Feleshi ni mzoefu wa Idara ya Mahakama na usimamizi wa sheria kwa jumla, hivyo hana tatizo katika nafasi ya Mwanasheria Mkuu.

Ila labda kuna ubishi utakaoendelea kuhusu Profesa Makame Mbarawa, ambaye alishindwa kupita katika uchaguzi mkuu 2015 halafu Dk. John Magufuli akamteua kuwa mbunge na kumrudisha serikalini kama waziri. Mengine ni mapito tu, ila Rais Samia amedhihirisha kumwamini pia.

Anachokiainisha Rais Samia katika maelezo baada ya kuwaapisha ni kuwa ametumia miezi sita iliyopita kuangalia wanachotenda mawaziri, anasema 'wanamsoma na yeye anawasoma.' Ina maana kuwa mabadiliko hayo ni matokeo ya kusoma nia za wasaidizi wake na kuangalia utii wao unaelekea wapi, kama wanajitahidi kutekeleza maagizo yake au wanaungana katika vikundi tofauti na kutekeleza yale wanayoyajua wao.

Malalamiko yalikuwa yameenea maeneo mengi, watu wakianza kulegeza kamba au kukaza kamba za sera, ambazo siyo zile alizoelekeza Rais Samia; mpaganyiko wa utawala unaoendana na dhana ya katiba mpya, ambako Rais anakuwa amepunguziwa madaraka na watendaji hawaingiliwi.

Rais Samia ametamka wazi, kuwa walioteuliwa watekeleze maagizo yake na siyo watunge au kufuata sera wanazotaka wao, wakitazamia kuwa hii ni 'serikali poa.' Ni kama vile aliahidi kuendelea kupima utendaji serikalini, alete mabadiliko mengine akiona inahitajika.

## Kinachowatofautisha wasajili vyama vya siasa nchini

**INATOKA UK.11**

na hata wenyeviti wa serikali za mitaa na vitongoji katika mikoa mbalimbali nchini.

"Upinzani ulikuwa na nguvu na hata watu walikuwa wakihama CCM kujiunga nao. Msajili Tendwa alipochukua nafasi, aliendelea kuvilea," anakumbusha.

Anasema yapo mambo ambayo Tendwa alishauri kwa lengo la kuimarisha vyama, lakini hayakutekelezwa hasa kwenye suala la ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992, kuhusu kufanya mikutano bila kuzuiwa.

"Pamoja na vikwazo hivyo, upinzani uliendelea kutimiza majukumu yake ingawa kwa sasa ni kama haupo tena, wapinzani wamebaki wachache, hawana nguvu tena kama zamani," anasema.

Katibu Mkuu mstaafu wa Chama cha TLP, Nancy Mrikaria, anasema pamoja na ukweli kwamba wasajili hao wamefanya kazi kwenye ofisi moja, wanatofautiana kiutendaji.

Kwa mtazamo wake, anaona Liundi hakuwa kiongozi wa kuchukua uamuzi wa haraka, bali alikuwa anajipa muda wa kufikiri kuhusu madhara ya uamuzi wake.

"Pamoja na kwamba alisimamia vyama vya siasa, alikuwa anatoa muda kwa vyama ambavyo aliviona vina upungufu wa kisheria na ufuatiliaji wake ulikuwa wa taratibu na upole," anasema Mrikaria.

Kuhusu Tendwa, Mrikaria anasema anasema alikuwa mkali kwa vyama vyenye upungufu na alitoa muda wa maboresho na hakuwa mwepesi kufuatilia au kwenda kwenye ofisi za vyama kuvifuta.



George Liundi. **PICHA: MTANDAO**

"Alisubiri kupelekewa taarifa ofisini kwake na alifuta vyama viwili, ambavyo ni People's Party (TPP) na PONA, lakini Mutungi yuko makini zaidi anafanya kazi kwa nadharia na vitendo na ni mwepesi kubaini upungufu na kutoa maelekezo kwa chama husika," anafafanua.

Mrikaria anasema msajili huyo amefuta vyama ambavyo vilishindwa kukidhi matakwa ya sheria na anaendelea kuvishughulikia ambavyo havifuati sheria na ni mwepesi kutembelea ofisi za vyama vya siasa.

"Usimamizi huo anaufanya kwa kushirikiana na vyama kwa karibu na kutoa muda wa kutosha wa kufanya marekebisho na ishindikana, sheria inafuata mkondo wake kwa kufuata vyama, ambavyo havifuati sheria," anasema.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Addo Shaibu, anasema utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa unategemea sheria, lakini pale kunapokuwa na udhibiti mkali, analaumiwa Msajili.

"Wakati wa Liundi na Tendwa kulikuwa na sheria ambayo haikuwa na udhibiti sana kama ilivyo sasa, ambapo kila jambo ambalo chama kinataka kufanya hata vikao vya ndani, lazima msajili aambiwe," anasema Shaibu.

Anasema Sheria ya Vyama vya Siasa ndiyo inayotoa taswira ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na pale inapokuwa kali, msajili ataonekana ni mkali na kumbe kinachosababisha ni sheria zilizopo.

"Sioni utofauti wa utendaji wa ofisi hiyo kuanzia kwa msajili wa kwanza hadi aliyepo sasa.

"Ninachokiona ni kuongezeka kwa sheria zinazodhibiti vyama, ambazo miaka ya nyuma hazikuwapo," anasema.

STERGOMENA TAX

# Ni maarufu kuvunja miiko

## • Wa kwanza Katibu Mtendaji SADC, Wizara Ulinzi



Stergomena Tax Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akila kiapo. **PICHA: IKULU**

**Na Christina Mwakangale**

STERGOMENA Tax ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akiwa ni mwanamama wa kwanza tangu uhuru, kushika wadhifa huo.

Katika kuonyesha kuwa siyo jambo lililozoeleka, hotuba anayoitoa Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa uapisho wake na mawaziri wengine anasema:

"Katika mabadiliko haya nimeamua kuvunja mwiko wa muda mrefu ya kwamba wizara ya ulinzi, lazima akae mwanaume mwenye misuli yake. Lakini kazi ya waziri si kupiga mizinga au kushika bunduki ni uratibu na kusimamia sera".

Waziri huyu wa ulinzi ana historia ya kuvunja mwiko. Ndivyo ilivyokuwa kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika-SADC Dk Stergomena kuanzia Septemba 01, 2013, aliteuliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi katika kikao cha 33 kilichofanyika Lilongwe, Malawi kuwa mtendaji mkuu wa chombo hicho na kula kiapo rasmi Agosti 2013.

Aliingia katika historia ya SADC akiwa Katibu Mtendaji wa sita lakini, mwanamama wa kwanza kukiongoza chombo hicho.

Stergomena, aliyeteuliwa kuwa waziri Jumapili iliyopita, anaongeza idadi ya viongozi wanawake wanaoongoza wizara nyeti na muhimu, ambao wamepata fursa hiyo wakati huu wa awamu ya sita.

Rais Samia anasema amempeleka kuongoza wizara hiyo si kwa sababu ya kuvunja mwiko huo, lakini kutokana na upeo wake mkubwa alioupata akiwa Katibu wa SADC.

"Alikuwa anasimamia vyema masuala ya usalama wa ndani ya Kanda," anasema Rais.

Stergomena (61) anaungana na viongozi wanawake, ambao wapo kwenye baraza la mawaziri akiwamo Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Prof Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu) Jenista Mhagama, Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima pamoja na Ummy Mwalimu anayeongoza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).



Wengine walio kwenye baraza hilo ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Liberata Mulamula pamoja na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Dk. Ashatu Kijaji.

Dk. Kijaji naye amaeandika historia, kuwa waziri wa kwanza mwanamama kushika wizara hiyo, akichukua nafasi ya Dk. Faustine Ndugulile.

Rais Samia ameihamishia Idara ya Habari katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hivyo wizara mpya itafahamika kama Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Kilichopo mbele yake Dk. Kijaji ni pamoja na kurejesha uhuru wa vyombo vya habari huku serikali ikiyafungia magazeti mawili ndani ya kipindi kifupi.

Magazeti hayo ni UHURU lilofungiwa kwa wiki mbili kuanzia Agosti 12 , 2021 na Raia Mwema ambalo kuanzia Septemba 6, 2021 lilisitishiwa leseni ya uchapishaji kwa siku 30.

Akiwaapisha mawaziri hao juzi jijini Dodoma, baada ya kuwateua Jumapili kufuatia mabadiliko madogo ya baraza la mawaziri, ambao ni Dk. Stergomena, Dk. Ashatu, Profesa Makame Mbarawa anayeongoza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na January Makamba Nishati, Rais Samia, anatoa neno mahususi kwa Waziri wa Ulinzi.

"Nimemchagua kwa upekee mkubwa hata katika kusimamia usalama katika ukanda hasa katika sekta ya ulinzi, yeye anajua tuna askari wangapi waliopo DRC, Msumbiji, atamsaidia vizuri Mkuu wa Majeshi katika upande huo."

**HISTORIA KIUONGOZI**

Ni mwanamama wa kwanza kuoingoza SADC. Tangu kuanzishwa kwa jumuiya hiyo mwaka 1980, Dk. Stergomena anakuwa Katibu Mtendaji wa sita, lakini wa kwanza mwanamke. Jukumu hilo alilimaliza Agosti 31 mwaka huu na kuandika tena historia ya kuwa mwanamama wa kwanza kuongoza wizara nyeti ya ulinzi.

Katika kazi hiyo aliyoianza tangu mwaka 2013, awamu yake ilikuwa ya muda wa kuangalia mafanikio na changamoto tangu kuanzishwa taasisi hiyo ya ushirikiano mwaka 1980.

Katika uongozi wake Katibu Mtendaji huyo, alifanikisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuandaliwa Mkakati wa Maendeleo wa SADC Development Vision 2050 .

Stergomena alizaliwa mwaka 1960. Ni msomi mwenye shahada ya uzamili ya falsafa ya maendeleo ya kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha Tsukuba cha Japan akisoma kuanzia 1995 hadi 1997.

> Nimemchagua kwa upekee mkubwa hata katika kusimamia usalama katika ukanda hasa katika sekta ya ulinzi, yeye anajua tuna askari wangapi waliopo DRC, Msumbiji, atamsaidia vizuri Mkuu wa Majeshi katika upande huo.

Kuanzia 1987 hadi 1991 alisoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Kabla ya hapo mwaka 1984, Stergomena alisoma katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), mkoani Dodoma, akichukua diploma ya uongozi wa biashara ya kimataifa.

Pia, amehusika kwenye utengenezaji wa mipango hai ya maendeleo Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Amebobea katika uongozi, usimamizi wa ufadhili na misaada, vilevile diplomasia.

Stergomena amebobea katika nyanja ya kimataifa hususan diplomasia, mwezi uliopita alikuwa Katibu Mtendaji SADC, nafasi aliyoanza nayo tangu mwaka 2013.

Awali, Stergomena, kabla ya kuingia SADC kwa miaka minane kuanzia 2013 akiwa mtendaji mkuu, alikuwa wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka 2008.

Uteuzi huo kuwa Katibu Mtendaji wa Wizara ya Afrika Mashariki kipindi hicho, ulikuwa kupanda cheo, kwa kuwa kabla ya hapo, alikuwa Naibu Katibu Mtendaji wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Stergomena, ni mama wa watoto wawili, aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mtendaji wa Wizara ya Mipango mwaka 2006, akitoka kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ubora (BRU), katika Mpango wa Uimarishaji wa Maendeleo ya Biashara Tanzania (BEST), chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Aliwahi pia kufanya kazi katika Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF) kama mratibu na mshauri na kuanzia Mei mwaka 1991 hadi Aprili 2002, alikuwa mfanyakazi wa Wizara ya Fedha, akiwa mhusika mkuu wa usimamizi wa misaada na uratibu (AMC).

Akiwa Wizara ya Fedha, Stergomena alikuwa ofisa wa usimamizi wa fedha kabla ya mwaka 1993, alipokuwa ofisa mkuu wa dawati la Benki ya Dunia (BoT).

Mwaka 1995, alikuwa msimamizi mkuu wa dawati la Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

JUKWAA LA VIONGOZI

ALPHA CONDE

# Alijidai hayupo anayetosha kuiongoza Guinea

• Ametumbuliwa kisa? Kung'ang'ania ikulu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Guinea, aliyetumbuliwa na jeshi lake, Alpha Conde, alikuwa na jeuri akijisifia tena kwa kuwaambia wanahabari kuwa ndiye pekee mwenye uwezo na msuli wa kuiongoza Guinea Equatorial.

Anajinasibu kuwa hata jeshi haliwezi kumuondoa. Tambo hizo sasa ni historia, yuko nje ya ikulu tena kwa mtutu wa bunduki na ujeuri huo unauona kama upuuzi.

Conde anaondolewa kwenye mapinduzi ya kushtukiza ya kijeshi yaliyommaliza na kumtoa nje ya hatamu yake ya kuongoza nchi ikiwa na utata baada ya kuupata uongozi uliobadilisha katiba.

Chini ya mwaka mmoja baada ya kushinda muhula wa tatu uliogubikwa na maandamano na ukandamizaji mkali, dhidi ya upinzani katika taifa hilo la magharibi mwa Afrika.

Conde, anatumbuliwa baada ya kuzuiliwa na wanajeshi wa kikosi maalum (GFS) mnamo Septemba 5, saa kadhaa baada ya kuripotiwa kufyatuliana risasi kwa karibu baina ya wanajeshi na walinzi kwenye makazi ya rais huko Conakry.

Kamanda wa GFS Kanali Mahamady Doumbouya, anathibitisha kuchukua serikali kupitia runinga ya serikali na kuahidi kusimamia mabadiliko ya uongozi kwa njia ya amani

Kikosi maalumu cha jeshi kiliingia ikulu na kumuondoa mkongwe huyo mwenye miaka 83, ambaye alikuwa anaendelea kula kuku kwenye ikulu ya Conakry bila kufikiria kung'atuka.

Licha ya kusema hata jeshi haliwezi kumundoa, kiongozi mpya wa kijeshi kanali Mamady Doumbouya, anajitokeza kwenye vyombo vya habari akiwa amevaa bendera ya Guinea , akitangaza rasmi kuwa ndiye kiongozi mpya wa taifa hilo.

Mapinduzi ya Guinea yameitumbukiza nchi hiyo kwenye hali ya kukosa amani na machafuko yanayoichagiza jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) kutishia kuiwekea vikwazo nchi hiyo inayozalisha madini ya bauxite kwa wingi duniani, ambayo yanatumiwa kutengeneza aluminium.

Mwaka 2010 Conde alitangazwa kuwa Rais wa kwanza wa Guinea aliyechaguliwa kidemokrasia na ushindi wake ukaonekana kuwa umemaliza kiza kinene cha uongozi wa madikteta Sekou Toure na Lansana Conte, waliokaa madarakani kwa miaka 50 Toure akiishi Ikulu miaka 26 na Conte 24.

Conde alichaguliwa kuongoza kwa awamu ya pili kuanzia 2015, lakini alizidi kuchukiwa na Waguinea hasa alipolazimisha kufanyika mabadiliko ya katiba kwa kusaidiana na Russia iliyokuwa inamuunga mkono.

Baada ya marekebisho hayo ya katiba, Conde alijiingiza kwenye mgogoro wa kikatiba uliomwezesha kuwa mgombea wa urais kwenye awamu ya tatu, kwenye uchaguzi wa Oktoba 2020 na kuibuka mshindi.



Kanali Mahamady Doumbouya kiongozi mpya wa kijeshi wa Guinea. **PICHA ZOTE: MTANDAO**


Aliyekuwa Rais wa Guinea, Alpha Conde.

> Mkiangalia hali za barabara zenu, hospitali zetu utajua kuwa huu ndiyo wakati wa kuamka na kufanyakazi. Tuamke na tulitetee taifa letu.

### CONDE ALIJITIA KITANZI

Mwanahabari Sidy Yansane, ambaye pia ni mchambuzi jijini Conakry, anasema Conde, alijitia mwenyewe kitanzi , alichokipanda alikivuna na amejiletea mwenyewe anguko lake.

"Conde alikuwa hakubaliki, hata kama walimpigia kura. Lakini kwa awamu hii ya tatu alikwenda mbali alivuruga ....."anasema mchambuzi huyo.

### UONGOZI MPYA

Katika hotuba yake aliyoitoa kwa taifa karibuni, Doumbouya, anasema kuondolewa kwa Conde' kulikuwa lazima na akaendelea kulaumu kuwa uongozi wake umehusika na umaskini nchini Guinea, rushwa na ufisadi , uongozi mbaya na kukosekana maendeleo.

Doumbouya anasema mabadiliko katika nchi hiyo na mifumo ya uongozi wa taasisi na vyombo vya dola vilihitajika kwa namna zote.

"Mkiangalia hali za barabara zenu, hospitali zetu utajua kuwa huu ndiyo wakati wa kuamka na kufanyakazi. Tuamke na tulitetee taifa letu," anasema Doumbouya.

Licha ya kusema maneno hayo hakueleza ni lini serikali ya mpito itachukua nafasi yake na kuongoza taifa hilo, ambalo linaelezwa kuwa lina kazi ngumu kujiondoa kwenye mkwamo wa kiuchumi.

"Wakati huu, watu wana kila sababu ya kufurahia. Wanashangilia kuondoka kwa Conde ,"

Ni jambo jema wananchi tutapenda kuona mambo bora yakifanyika wakati huu kutoka kwa viongozi wa mapinduzi na suala la kuwa na serikali na uongozi wa mpito."

Ubinafsi umekwisha. Tutaweka mpango wa mpito ulio wazi na unaojumuisha watu wote. Tutaweka mfumo ambao [sasa] haupo," Doumbouya anasema wakati akiwa amezungukwa na maafisa wa GFS wenye silaha waliojifunika bendera ya Guinea.

Kanali Doumbouya, ambaye anasemekana alipata mafunzo ya kijeshi nchini Ufaransa, anaonekana kuwa katika uongozi wa kikosi cha jeshi kilichochukua madaraka nchini Guinea, kwa jina la National Committee for Rally and Development (CNRD), inasema BBC.

### WASIFU WA DOUMBOUYA

Mengi hayajajulikana kuhusu maisha ya utotoni ya Doumbouya, isipokuwa ni wa kutoka kabila la Malinke kama Rais Conde na anatoka Mkoa wa Mashariki wa Kankan wa Guinea.

Alikuwa huko Forecariah, magharibi mwa Guinea, ambapo alihudumu chini ya ofisi ya uchunguzi na huduma za ujasusi.

Doumbouya anaripotiwa kusoma katika chuo cha vita huko Paris, Ufaransa na ana uzoefu wa miaka 15 wa kijeshi, ambayo ni pamoja na misheni nchini Afghanistan, Cote d'Ivoire, Djibouti, Jamhuri ya Afrika ya Kati na ulinzi wa watu mashuhuri Israeli, Cyprus , Uingereza na Guinea.

Kanali huyo anasemekana "amekamilisha vyema" mafunzo ya wataalam wa ulinzi wa kiutendaji katika Chuo cha Usalama cha Kimataifa huko Israeli, kozi ya mafunzo ya makamanda wa shule huko Senegal.

Alihudumu kama mwanajeshi wa kigeni yaani 'legionnaire' katika jeshi la Ufaransa hadi 2018, wakati Conde alipomtaka arudi Guinea kuongoza GFS, iliyoanzishwa mwaka huo.

### HOFU DHIDI YAKE

Tangu 2018, kumekuwa na ripoti kadhaa kwenye vyombo vya habari vya Guinea zikitilia shaka sifa za Doumbouya.

Agosti 2021, gazeti la Friaguinee lilidai kwamba Dombouya alinyimwa uraia wa Ufaransa kwa sababu "mwenendo wake ulionekana kuwa kinyume na maadili na kanuni" za jeshi la Ufaransa. Ilihoji pia chanzo cha utajiri wa kanali huyo.

Wakati ikiripotiwa kuhusu mali kadhaa zinazodaiwa kuwa ni za kanali Doumbouya, Friaguinee liliuliza: "Ofisa huyu, ambaye anapokea mshahara wa chini dola 500 ( milioni 1.6) anawezaje kujenga majengo haya yote?"

Mnamo Mei, Doumbouya alikuwa miongoni mwa maofisa 25 wa Guinea waliowekewa vikwazo vya Umoja wa Ulaya EU, kwa ukiukwaji wa haki za binadamu.

Hatua iliyochukuliwa kufuatia uvumi wa kuzuiliwa kwa watu katika kambi ya Dubreka magharibi mwa Guinea, lakini vikwazo hivyo vilifutwa. Doumbouya pia alikuwa akipinga wizara ya ulinzi ya Guinea kusimamia kikosi cha GFS kilichoundwa na Conde.

**BBC /ALJAZEERA**



# Agizo shule ya mfano kukamilika Desemba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, ameagiza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano iliyoko Iyumbu jijini Dodoma kukamilika Desemba mwaka huu, ili kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2022.

Kipanga aliyasema hayo juzi alipokuwa akikagua ujenzi wa shule hiyo na Chuo cha Ufundi cha Kanda ya Kati kinachojengwa Nala jijini hapa.

Alisema ujenzi huo unafanywa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (Suma JKT) kuhakikisha wanakamilisha ujenzi huo ili mwakani wanafunzi waanze kusoma.

Kipanga alisema shule hiyo ina gharimu Sh. bilioni 17.1.

"Tunampongeza Rais kwa kujali sekta ya elimu, hii shule awali ilipangwa kukamilika Februari 2022. Naagiza ikamilike Desemba ili ifikapo Januari mwakani ianze kuchukua wanafunzi wa sekondari," alisema.

Aidha, alisema tangu serikali ilipopitisha utaratibu wa elimu bila malipo kuna idadi kubwa ya wanafunzi wanaopata fursa ya kuandikishwa shule na hivyo kuongeza mahitaji ya shule na vyumba vya madarasa.

Akitoa taarifa ya ujenzi huo, Naibu Kamanda wa Operesheni JKT, Suma Meja Geoffrey Ngole, alisema ujenzi ulianza Julai 2020 na utakamilika Februari mwaka 2022.

"Tumepokea maagizo ya Naibu Waziri ya kukamilika kazi ifikapo Desemba, tunaongeza nguvu kazi na tutafanya kazi usiku na mchana ili tumalizekwa muda uliotajwa na Naibu Waziri," alisema Meja Ngole.

Alisema ujenzi huo upo katika sehemu tano ikiwamo jengo kuu, bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 na bweni la wavulana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500, bwalo, nyumba 10 za watumishi, jengo la utawala, nyumba za walimu, viwanja vya michezo na matangi ya maji.

Akiwa katika Chuo cha Ufundi Nala, Kipanga alisema kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,000 na awamu ya kwanza kitachukua wanafunzi 1,500.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 17.9 na ujenzi ulianza mwezi Juni, mwaka huu na utachukua miezi 18 kukamilika.

Hata hivyo, alisema lengo la chuo hicho ni kuwezesha vijana wengi kupata ujuzi,kuzalisha vijana wenye ujuzi wa kati.

Kipanga alisema serikali imejipanga kujenga vyuo vya ufundi katika kanda zote nchini kadri bajeti itakavyoruhusu.

# AfDB, DUWASA wajadili ufadhili ujenzi wa bwawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (DUWASA), imeanza mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili kufadhili ujenzi wa bwawa la Farkwa litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 128 kwa siku.

Hatua hiyo inalenga kuondoa upungufu wa maji uliopo kwa sasa wa lita milioni 37.

Akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini hapa juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph, alisema benki hiyo imeonesha nia ya kufadhili sehemu ya mradi huo.

"Kuanzia Septemba 13 hadi 25, mwaka huu tutakuwa na majadiliano nao (AfDB), ili wanapokwenda kwenye bodi yao na taratibu zote zinazohusu kupata fedha za mradi huo wenye masharti nafuu zinakuwa zimekamilishwa."

"Sisi upande wetu DUWASA tumekamilisha masuala yote yaliyotakiwa kukamilisha na wizara ikiwamo fidia zote zilizopaswa kufanyika katika eneo la bwawa zimekamilika, kuhamisha makaburi na vitu vyote vilivyopaswa kuhamishwa tayari vimekamilishwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ujenzi wa bwawa hilo ni juhudi za muda mfupi za kupata maji, ili kuondoa upungufu uliopo na kuhudumia Wilaya ya Chemba, Bahi na Chamwino.

"Pia kuna mradi wa Ziwa Victoria ambao upo kwenye hatua ya kufanya upembuzi yakinifu ili kuhakikisha unatekelezwa kwa kutoa maji Ziwa Victoria kuja Dodoma," alisema.

Awali, alisema mwaka 2016, Dodoma ilikuwa na watu chini ya 350,000 ambao walihudumiwa na mamlaka hiyo na uhitaji wa maji ulikuwa lita milioni 48 ambayo yalijitosheleza, lakini baada ya kuongezeka kwa watu kufuatia ujio wa serikali, watu wameongezeka hadi zaidi ya 500,000 na hivyo mahitaji kwa sasa ni lita milioni 103.

"Kulitokea kama tetemeko la ardhi chini ya ardhi na kupunguza uwezo wa baadhi ya visima kuzalisha Mzakwe na Waziri aliingilia kati tukapata fedha za kuchimba visima vitatu vikubwa Mzakwe vyenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 13 na kufikia lita milioni 61.5 kwa siku, hali hiyo ilipunguza makali ya mgao kwa kuwa tulikuwa tuna uwezo wa kuhudumia wananchi kwa saa tano sasa hivi saa 10," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa uwezo uliopo katika vyanzo vyote vya kuzalisha maji ni lita milioni 66 kwa siku, na mahitaji ni lita milioni 103, hivyo upungufu ni lita milioni 37 ndio unasababisha kuwapo na mgao wa maji ambapo kila eneo linapata mara tatu kwa wiki.

Alisema kwa sasa pia kuna mradi unatekelezwa wa kutoa maji chanzo cha Ihumwa ambapo visima vitano vimechimbwa ili kuhakikisha maeneo ya pembezoni Kisasa, Nzuguni, Njedengwa na kwasasa umefikia asilimia 90 ambapo serikali imeshatoa Sh. bilioni 1.3 ili kukamilisha kabla ya Oktoba mwaka huu.

"Kwa Chamwino tumechimba visima vina uwezo wa kuzalisha lita milioni 15 kwa siku na uhitaji ni lita milioni 3, hivyo wana akiba ya maji ya kutumia kwa miaka 10 ijayo,"alisema.

Aidha, alisema Chamwino ni miongoni mwa miji inayonufaika kwenye mradi wa miji 28 na fedha za mradi huo zitatumika kusambaza maji kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa yanayohudumiwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, akizungumza kwenye hafla ya utiaji saini makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na China kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Uwanja wa Ndege Msalato kujengwa awamu 2

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeingia makubaliano na mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kiwanja kipya cha ndege cha kimataifa Msalato unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, akitoa taarifa fupi ya mradi wa ujenzi wa kiwanja hicho jana jijini Dodoma, alisema kitajengwa kwa awamu mbili.

"Awamu ya kwanza inahusisha kazi kuu mbili ambazo ni ujenzi wa barabara ya kuruka ndege na ujenzi wa majengo ikiwamo jengo la abiria."

"Mkandarasi aliyepatikana kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege ni Sinohydro Corporation Limited in JV with M/s Beijing Sino-Aero Construction Engineering Co., Ltd and M/s China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation CO.,Ltd kutoka China," alisema Mtivila.

Pia alisema awamu ya kwanza ya ujenzi huo itakapokamilika, kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 1.5 kwa mwaka.

"Mheshimiwa waziri, awamu ya pili ya mradi itatekelezwa kwa kutegemea mahitaji yatakayojitokeza ndani ya kipindi cha miaka 20, baada ya ujenzi wa awamu ya kwanza kukamilika," alisema Mtivila.

Alisema AfDB, itatoa jumla ya Dola milioni 329.47 na Serikali ya Tanzania itagharamia Sh. bilioni 127, ambapo fedha zitakazochangiwa na serikali ni pamoja na malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi.

Kadhalika, alisema ujenzi wa kiwanja hicho utakapokamilika utarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia katika jiji la Dodoma na kati ya Tanzania na nchi mbalimbali, kukuza utalii, uchumi na kuongeza ajira.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliagiza TANROADS kuhakikisha inasimamia ujenzi huo ili ukamilike kwa wakati na kwa viwango.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa uwanja huo kutawezesha kutua kwa ndege kubwa kama Airbus pamoja na Dreamliner katika Mkoa wa Dodoma.

"Pia kiwanja hiki kitafungua fursa mbalimbali za kiuchumi kwa mkoa wa Dodoma, hivyo TANROADS mhakikishe kuwa mkandarasi mnamsimamia ipasavyo ili kumaliza kazi hii kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa," aliagiza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, alisema kitendo cha wizara hiyo kutiliana saini mkataba wa ujenzi kimejibu maswali mengi yalikuwa yakihojiwa na wananchi juu ya hatima ya uwanja huo.





# Serikali yaombwa kuunda chombo kushughulikia migororo wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeombwa kuunda chombo kimoja cha kushughulikia migogoro ya wafanyakazi wote bila kujali kuwa wanatoka kwenye sekta ya umma ama binafsi ili kuondoa tofauti iliyopo baina ya watumishi hao.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Ufundi Stadi, Habari na Ushauri (RAAWU), Winston Makere, alitoa ombi hilo juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalumu kwa viongozi na wawakilishi wa matawi ya chama hicho.

Alisema kwa sasa migogoro ya wafanyakazi wa sekta binafsi na wa umma inashughulikiwa na vyombo tofauti huku akidai kuwa utatuzi wa migogoro ya wafanyakazi wa sekta binafsi na waajiri wao mlolongo wao ni mfupi kuliko wa sekta ya umma.

Alisema endapo kitaundwa chombo kimoja cha kushughulikia, migogoro hiyo itaepukika na tofauti kati ya wafanyakazi wa sekta hizo na itakuwa inatatuliwa kwa haraka na kuwapunguzia mzigo wafanyakazi.

"Kwa sasa mtumishi wa umma anapokuwa na mgogoro wa kinidhamu na mwajiri wake wanapelekana kwenyeTume ya Utumishi wa umma, ikishindikana huko anakata rufani kwa Rais na baadaye Mahakama ya Rufani, lakini wafanyakazi wa sekta binafsi wenyewe wanapelekana na waajiri wao kwenye Mahakama ya Usuluhishi na kuendelea kwenye mahakama zingine na hivyo mchakato wao ni mfupi," alisema Makere.

Katika hatua nyingine alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya waajiri kutovitaka vyama vya wafanyakazi kwenye maeneo yao ya kazi wakiamini kuwa vyama hivyo ni vya wapinzani wao jambo ambalo alisema ni dhana potofu. Alisema lengo la vyama vya wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi ni kuweka daraja kati ya mwajiri na wafanyakazi na kwamba utaratibu huo ni mzuri kwenye kuongeza ufanisi wa kazi.

Hata hivyo, alisema baadhi ya taasisi za umma hazijaunda mabaraza na wala haziitishi mabaraza ya wafanyakazi jambo ambalo ni takwa la kisheria na hivyo akaiomba serikali kuzilazimisha taasisi hizo kutekeleza takwa hilo. Akifungua mafunzo hao, Naibu Spika Dk. Tulia Ackson alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa viongozi hao wa matawi ya RAAWU kwa kuwa yanawasaidia kuzijua sheria za wafanyakazi pamoja na namna ya kuongoza vyama hivyo.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kusikiliza kwa makini wanachofundishwa ili na wao wawapelekee wenzao kwenye matawi yao ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu mambo hayo yanayofundishwa.

Alisema mafunzo hayo pia yanawasaidia wafanyakazi na viongozi wa vyama hivyo kujiandaa kustaafu vyema kutokana na kuwa na kipengele cha kujifunza utawala wa fedha pamoja na ujasiliamali ambao alidai wakijifunza watajua namna ya kutunza fedha na usahihi wa matumizi.

"Haya mengine yanayohusu mambo ya kisheria ninayachukua na nitayafikisha kwenye maeneo yanayohusika ili yashughulikiwe, lakini pia wabunge wanaowawakilisha wafanyakazi kule bungeni nitakaa nao ili tuone namna ya kushughulikia mambo haya," alisema Dk. Tulia.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa vyama hivyo vya wafanyakazi kuorodhesha majina ya waajiri ambao hawaitishi mabaraza ya wafanyakazi ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao kwa maelezo kuwa wanakiuka sheria.



Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Ufundi Stadi, Habari na Ushauri (RAAWU), Winston Makere (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo maalumu kwa viongozi na wawakilishi wa matawi ya chama hicho, jijini Mbeya juzi. Kulia ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson na Mkuu wa Chuo cha Wafanyakazi Tanzania (OTTU), Hezron Kaaya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mwezi mmoja mradi wa maji ukamilike

**Na Nebart Msokwa,** KYELA.

SERIKALI imepewa mwezi mmoja kukamilisha Mradi wa Maji Mababu wilayani Kyela ili zaidi ya wananchi 5,000 wa kata za Mababu, Matema na Mwakwale, waanze kunufaika na huduma hiyo muhimu.

Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa, Luteni Josephine Mwambashi, alitoa agizo hilo juzi baada ya kukagua mradi huo na kubaini kuwa wananchi wanaolengwa kunufaika hawapati huduma ipasavyo.

Alisema ujenzi wa mradi huo unaendelea vyema japokuwa kasi yake ya ujenzi bado hairidhishi na kuitaka serikali kuongeza kasi ili mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Septemba uwe umekamilika na wananchi waanze kunufaika nao.

Alisema mradi huo ni miongoni mwa yenye faida kwa wananchi wa maeneo hayo na kwamba ni lazima serikali iongeze nguvu ya kuujenga ili ukamilike haraka.

"Nimeridhika na utekelezaji wa mradi huu na ukikamilika naamini utasaidia sana wananchi wa maeneo haya, lakini sasa naiagiza serikali ihakikishe mradi huu unakamilika mwishoni mwa mwezi huu, sasa hivi wananchi wanapata huduma, lakini sio kwa kiwango kinachotarajiwa," alisema Mwambashi.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa Wakala wa Maji vijijini (RUWASA) wa Wilaya ya Kyela, Mhandisi Tanu Deule alisema mradi huo ni wa kusukuma maji kwa njia ya mseleleko ambao gharama yake ni ndogo kuliko inayosukumwa kwa mashine.

Alisema ulianza kuboreshwa mwaka 2019 baada ya kubaini kuwa ulikuwa unawahudumia wananchi wachache kuliko uhalisia wa mahitaji ya wananchi na kwamba uliwekwa jiwe la msingi na mbio za Mwenge za mwaka huo. Alisema baada ya kukamilika wananchi wanaonufaika wataongezeka kuliko wanaonufaika kwa sasa na kwamba kwa sasa mradi huo uko katika hatua nzuri.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi alisema mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 500 na kutokana na maagizo ya kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa watahakikisha wanaongeza usimamizi.

Alisema wataendelea kuwasimamia RUWASA ili wakamilishe haraka kabla ya mwezi Oktoba, mwaka huu huku akidai kuwa kwa sasa wananchi wanapata maji kwa mgawo kutokana na kutokamilika.

"Tutasimamia kwa nguvu zote ili kuhakikisha unakamilika mapema na wananchi wanaanza kupata huduma, lakini kwa sasa wananchi wanapata huduma japo kuwa wanapata kwa muda mchache na wanapata kwa mgawo," alisema Mahundi.

Ukiwa wilayani Kyela, Mwenge wa Uhuru uliweka mawe ya msingi katika miradi mitatu, kukagua miradi miwili na kuzindua kiwanda cha kukamua mafuta ya mawese kinachomilikiwa na kikundi cha watu wenye ulemavu katika kijiji cha Ipinda.

# Wananchi wajitolea kujenga kilomita 2 za barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Iwambi, Halmashauri ya Jiji la Mbeya wametumia nguvu zao kujenga barabara yenye urefu wa kilomita mbili ili kurahisisha mawasiliano ya barabara kati ya eneo lao.

Wananchi hao wameiomba serikali iwasaidie utaalam wa kuweka mitaro na makaravati ya kupitisha maji ili barabara hiyo idumu kwa muda mrefu na wameijenga barabara hiyo kwa kuchangishana fedha kwa ajili ya kukodi mitambo.

Wakizungumza na na waandishi wa habari juzi wananchi hao walisema waliamua kujenga barabara hiyo baada ya kuona wanapata shida ya kusafiri kutoka katika eneo hilo kuunganisha katika barabara kuu.

Charles Mtagwaba, ambaye ni miongoni mwa wakazi wa eneo hilo alisema awali katika eneo hilo hapakuwa na barabara isipokuwa palikuwa na wigo uliokuwa unatenganisha shamba la mifugo na maeneo ya wananchi.

Alisema baada ya wananchi kuongezeka katika eneo hilo waliamua kuanza kulima barabara hiyo kwa kutumia jembe la mkono lakini walikuwa wanashindwa kufanikiwa kwa sababu mafuriko yalikuwa yanazoa udongo na kusababisha makorongo.

"Baadhi ya watu huku sasa hivi wana magari lakini sasa barabara imeharibika, mafuriko yalisababisha makorongo mengi sasa tumeona ni vema tuchangishane ili kuiboresha, sasa sisi tumeijenga lakini tunahitaji utaalamu kutoka serikalini ili mitaro iwe ya kisasa," alisema Mtagwaba.

Naye John Chigazi, alisema wamejenga barabara hiyo kwa kiwango cha kawaida na wanaiomba serikali iwasaidie kuboresha zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka vifusi vyenye ubora na mitaro imara ya kitalaam.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kuunganisha makazi yao na barabara kuu eneo la katikati ya Jiji la Mbeya ambako ndiko huduma nyingi muhimu zinapatikana.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na vijijini (TARURA) wa Jiji la Mbeya, Mhandisi Seleman Mziray alisema barabara imo kwenye mtandao wa barabara wa wakala huo na kuwataka wananchi hao kuendelea kufuata utaratibu.

Alisema wananchi hao wanatakiwa wafuate utaratibu wa kuomba ili barabara hiyo ianze kuhudumiwa na TARURA huku akiwapongeza kwa kuamua kuijenga.

Aliwataka kuanza mchakato wa kuomba barabara hiyo kwa kuanza na mikutano ya mitaa yao kisha wawasilishe mihutasari yao kwenye kata kabla ya kufikishwa kwenye vikao vya halmashauri.



# Lugha kikwazo kwa watembeza watalii

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KUKOSEKANA kwa watembeza watalii wazawa kumesababisha kazi hiyo visiwani Zanzibar kufanywa na raia wa kigeni (wazungu) baada ya kukosekana kwa wazawa wenye kufahamu vizuri baadhi ya lugha zinazotumiwa na watalii.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mussa Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Sulubu Kidongo, aliyetaka kujua sababu ya wageni kutembeza watalii kazi ambayo awali ilitakiwa kufanywa na wazalendo.

Alisema sheria ya watembezaji watalii imetoa ruhusa kwa kampuni zinazoleta watalii nchini kuwatumia wageni kwa ajili ya kutoa maelezo kwa watalii kwa lugha inayofahamika zaidi.

Alisema suala hilo limejitokeza katika siku za hivi karibuni kwa kundi la watalii kutoka Russia waliofika nchini na watembezaji watalii wa kigeni walilazimika kutoa ufafanuzi kwa wageni katika maeneo waliyotembelea kwa lugha yao.

"Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli yapo makundi ya watalii wanaotembelea nchini katika vivutio mbalimbali hulazimika kuwaruhusu watembezaji wa kigeni kutoa ufafanuzi wa taarifa kwa lugha fasaha wanayoitumia na kutoa mfano watalii kutoka Russia waliruhusiwa kuwatembeza watalii hao," alisema.

**Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mussa Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Sulubu Kidongo, aliyetaka kujua sababu ya wageni kutembeza watalii kazi ambayo awali ilitakiwa kufanywa na wazalendo.**

# Serikali sasa kuimarisha mitaala vyuo vya ufundi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema imejipanga kuimarisha mitaala ya vyuo vya amali (ufundi), ili kwenda na wakati na mahitaji ya soko la ajira lilioko hivi sasa kwa vijana kujiajiri.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohamed Said, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Profesa Omar Fakih Hamadi, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuboresha vyuo vya amali.

Waziri huyo alisema wizara anayoiongoza imejipanga vizuri kuona kwamba mitaala ya vyuo vya amali inaboreshwa kwa kuongeza masomo zaidi yenye mahitaji ya soko.

Alisema mafunzo ya aina 17 yanatolewa na vyuo vya amali vilivyoko Mkokotoni, Mwanakwerekwe kwa Unguja na kwa Pemba ni vitongoji vya Daya.

Alisema mafunzo ya uvuvi wa kilimo cha mwani tayari yameanza kutolewa kufuatilia kuwapo kwa mipango ya kujengwa kwa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao hilo.

Aidha, alisema majengo ya maabara ya kusindika mazao ya baharini na mboga tayari yamejengwa ikiwa ni sehemu ya mradi wa ushirikiano na Serikali ya India.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, akijibu swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Marufuku uokotaji karafuu zinazoanguka'

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepiga marufuku uokotaji wa karafuu zinazoanguka chini maarufu kwa jina la 'mpeta' baada ya kubainika kuchangia kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kusababisha pia wanafunzi kutoroka shule.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa wizara hiyo, Omar Said Shaaban, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum Kaskazini Pemba, Shadya Suleiman, aliyetaka kujua sababu za serikali kupiga marufuku uokotaji wa karafuu zinazoanguka chini.

Alisema kumejitokeza matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika kipindi cha msimu wa mavuno ya karafuu na kundi hilo hujishughulisha uokotaji wa zinazoanguka chini.

Kadhalika alisema utafiti unaonyesha kwamba matukio hayo huongezeka katika msimu wa mavuno na wanawake na watoto ndiyo wengi wanaojitokeza katika kazi za kuokota karafuu hizo.

"Mheshimiwa Mwenyekiti Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepiga marufuku uokotaji wa karafuu zinazoanguka chini kwa sababu tumefanya utafiti na kubaini kuwapo kwa kasi ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na watoto kutoroka shule," alisema.

Aidha aliwataka wakulima wa karafuu kuongeza bidii kuhakikisha kwamba wanapata karafuu daraja la kwanza ili kupata kipato kikubwa.

Alisema kazi ya kupata karafuu daraja la kwanza masharti yake wakulima wengi wa karafuu wanayafahamu ikiwamo kuanika vizuri karafuu hizo na kukauka.

"Tunawaomba wakulima wetu kuhakikisha wanapata daraja la kwanza la karafuu ambapo masharti yake kukauka vizuri na kuzisafisha taka zote," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI

**ACTUARIAL SOCIETY OF TANZANIA** wanatangaza kupotea kwa Cheti Cha Usajili **Namba SO.15725** kilichotolewa na Msajili wa Taasisi za Kijamii

**Taarifa imetolewa Kituo cha Polisi kwa Kumb Na. DAR/GOG/ RB/437191/2021**

116458602

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.104 Of 2021**

**In the matter of the estate of the late PHILEMON FUNGO MGOHACHI Mahoma Makulu within Dodoma city**
**And**

**In the matter of the application for letters of Administration by JOSEPH P. FUNGO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 9/2021

**Dated at Dodoma this 14 day of 9/ 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

116458402

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.60 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the late PETER ELIANGIKUNDI MRIA of Area E within Dodoma Region**
**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOSEPH ELIANGIKUNDI MRIA**
**AMENDED PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION WHEN DECEASED DIED INTESTATE.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22 day of September 2021.
Dated at Dodoma this 07 day of September 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

116459602

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.... OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late VERIANI SAMUSON MAHINIJE of Ng'hong'honha Ward within City council of Dodoma.**
**AND**
**in the matter of an application for letters of administration by SIMONI HABELI KAMUNYA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of OCTOBER 2021.
**Dated at Dodoma this 13 day of September 2021**

13 day of September
RESIDENT MAGISTRATE

116459702

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI YA TALAKA NAMBA 6/2021**
**MARTHA SHAYO……………………MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MITATHI YA BRYCESON MCHARO…………………........MAJIBU MAOMBI**

Mahakama hii inawafahamisha kwamba mwombaji tajwa hapo juu amefungua shauri la Taraka namba 6/2021 katika Mahakama ya Wilaya Morogoro.
Shauri hilo limepangwa kutajwa mnamo tarehe 28 mwezi wa 9 mwaka 2021 saa 02:30 mbele ya Hakimu Richard Kasele asubuhi hivyo mjibu maombi unaombwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauiri litaanza kusikilizwa bila kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 14 mwezi 9 mwaka 2021

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MOROGORO**

116458502

---

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

## MAS & ASSOCIATES CO. LIMITED & COURT BROKER

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC)** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE LILILOTOKA TANGAZO HILI UWE UMELIPA DENI LAKO KAMA HAUTALIPA NDANI YA MUDA TULIOKUPA TUTAUZA NYUMBA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA ILI KUFIDIA DENI LOTE UNALODAIWA NA **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC).**

| NO | JINA | MALI ILIYOWEKWA DHAMANA | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | STEPHEN ELIKUNDA MTINDI | CT NO.23898-MBYLR, LO NO.379062, PLOT NO.192, BLOCK "TT" LUWAWASI / MKUZO AREA, SONGEA MUNICIPALITY I.N.O. ADEN BAHATI | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 2. | JOHN CHARLES MWELI | CT NO.13459-DLR, L.O. NO. 161048, PLOT NO. 29 BLOCK '13' WEST CHINANGALI DODOMA MUNICIPALITY INO CHARLES JOHN | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |

**MASHARTI YA MNADA:**

- UKAGUZI UNAANZA MARA BAADA YA TANGAZO HILI, MASHARTI YA MNADA:
- MNUNUZI ANATAKIWA KULIPIA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75% SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA NA HUKIKOSA KULIPA MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZOLIPA HAZITARUDISHWA.
- GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA ZA MALI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE
- MTEJA ATATAKIWA KULIPA FEDHA TASLIM SIO HUNDI.

**KWA MAWASILIANO**
**MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER**
**SIMU: 0712 667989**
**WOTE/ MNAKARIBISWA**

116459302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 94/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
Marehemu **HASSANI MUSTAPHA HIMBUKA** wa kijitonyama
Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi wa yaliyoletwa na **SHOMARI HASSANI HIMBUKA**

## TANGAZO

*(kanuni ya 5(2)ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri hlii endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 8 mwezi 10** mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
. wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
. marehemu hakuacha wosia
**Imetolewa leo tarehe 9 mwezi 9 mwaka 2021**

116452502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINLION INVESTMENT CO. LTD** INATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 494 ABN AINA YA KING LION. CHASSIS NAMBA LTBPK8BG8E2K08637.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MKB/ RB/172/2021.**

116459502

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**LAURENT PETRO NDOMELO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1882-0048** kilichotolewa na IHANAMILO SEKONDARI mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **MOR/PS/B.1/35/VOL CXX/X/80.**

116458202

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DIVISHENI YA KAZI**
**DAR ES SALAAM**
**MAOMBI YA MAREJEO NA. 177 YA 2019**
**BAINA YA**
**AZAM BAKKERIES LTD ........................................MLETA MAOMBI**
**NA**

RAMADHANI KUIRANGA.....MJIBU MAOMBI 1
JUMA MWIDARU.................... MJIBU MAOMBI 2
Stumai Jumbe................ MJIBU MAOMBI 3
Khamis Othman............ MJIBU MAOMBI 4
Rukia Rajabu.................. MJIBU MAOMBI 5
Emmanuel Senzighe............ MJIBU MAOMBI 6
Shani Kambangwa............MJIBU MAOMBI 7
Frank Rumisha............... MJIBU MAOMBI 8
Habiba Salim..................MJIBU MAOMBI 9
Fauzia Ramadhani............MJIBU MAOMBI 10
Zaina Hamadi................. MJIBU MAOMBI 11
Wema Mwakipesile...............MJIBU MAOMBI 12
Leonida Kashangaki.........MJIBU MAOMBI 13
Asma Saidi ..................MJIBU MAOMBI 14
Rehema Saidi .....................MJIBU MOMBI 15
Fatuma Mpunga..............MJIBU MAOMBI 16
Saumu Rashid .....................MJIBU MAOMBI 17
Ramadhani Twaha .........MJIBU MAOMBI 18
Khadija Kanyepe .........MJIBU MAOMBI 19
Mwantumu Sued ...............MJIBU MAOMBI 20
Amina Nyakunga ............MJIBU MAOMBI 21
Adam Ramadhani .........MJIBU MAOMBI 22
Mayasa Salum ............MJIBU MAOMBI 23
Bahati Odillo ............MJIBU MAOMBI 24
Habiba Abdallah .........MJIBU MAOMBI 25

**Kwa**
**RAMADHANI KUIRANGA NA WENZAKE 24**
**DAR ES SALAAM**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Rejea mada hapo juu.
Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 21 Septemba, 2021 saa 3:00 Asubuhi bila kukosa na utetezi wako pamoja na vithibitisho / vielelezo vyako vihusuvyo maombi yaliyofunguliwa dhidi yako na kuviwasilisha Mahakamani tayari kwa kusikilizwa maombi.
Fahamu kuwa kukosekana kwako siku hiyo iliyotajwa, maombi haya yatasikilizwa na kuamuliwa bila wewe kuwepo.

Imesainiwa hapa Dar es salaam siku ya Ijumaa tarehe 10 Mwezi September, 2021.

F. S. Kiswaga
KAIMU NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DIVISHENI YA KAZI

116341302

---

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kigali sasa usafiri mjini kati ni baiskeli

**Kigali, RWANDA**

MJI wa Kigali umeanzisha aina mpya ya kusafiri mjini humo kwa kutumia baiskeli ikiwa ni juhudi za Rwanda za kukabiliana na uchafuzi wa mazingira, kupunguza hewa ya kaboni katika miji na vituo vya miji inayokua.

Wasafiri watatumia baiskeli hizo kwa kupokezana katika mji mkuu Kigali kwa bei ya chini, ikilinganishwa na usafiri mwingine wa mjini.

Mjini Kigali, Mtaa wa Remera baiskeli nyingi zenye rangi ya kijani na njano zimeegeshwa katika kila kona ya barabara.

Wakazi wa mji huo wanapakua maombi maalumu kwenye 'Play Store' ya simu zao, ili kutumia baiskeli, alieleza kijana wa kike ambaye amekuwa akitoa maelezo kwa wapita njia wanaoshuhudia jinsi ya matumizi ya baiskeli hizo.

Kuna vituo 13 vya baiskeli mjini Kigali ambako pia kuna barabara maalumu za kuendeshea baiskeli.

Mtaa wa Remera karibu na uwanja wa mpira kuna vituo vingine na baadhi wameanza kutumia baiskeli hizi.

Kwa mjibu wa kampuni ya 'Gura Ride' inayosimamia mpango huo anayetaka baiskeli anaichukua katika kituo kilicho karibu na kisha shughuli zake kuiweka kwenye kituo kingine kilicho karibu na mwisho wa safari yake.

Hata hivyo kikwazo kilichopo ni kwamba bado kuna barabara chache za kuendeshea baiskeli mjini Kigali, pia milima iliyopo.

Wahusika wana majibu kwa vikwazo hivyo, Jerry Ndayishimiye ni ofisa wa GuraRide:

Meya wa Jiji la Kigali, Pudence Rubingisa, amesema lengo kubwa la mradi huu ni kukabiliana na uhalibifu wa mazingir, tunataka usafiri unaotusaidia kulinda uchafuzi wa mazingira, kusafiri bila kutumia magari, tutakaposafiri kwa kutumia baiskeli itakuwa faida kubwa kwa afya zetu kwa kupata hewa safi."

**BBC**




'Karibu tena shule' ni ujumbe uliopo kwenye wigo wa Shule ya PS 245 Brooklyn, jijini New York nchini Marekani, huku watoto wakiwasili shuleni kwa kusindikizwa na wazazi wao, juzi. Shule za umma zimefunguliwa na kuwarudisha mamilioni ya wanafunzi jijini humo, baada ya kufungwa kwa kipindi kirefu kutokana na corona. **PICHA: AP**

# Wanaharakati 227 wauawa duniani 2020

**New York, MAREKANI**

DUNIA iko katika hali mbaya kutokana na watetezi wa haki za binadamu kuwa walengwa katika visa mbalimbali.

Mwaka jana, wanaharakati 227 wa mazingira waliuawa. Haya ni kulingana na ripoti ya Shirika la Kimataifa la Global Witness.

Mashambulio hayo kila wakati yanahusishwa na visa vya unyonyaji mwingi wa maliasili na yamekithiri katika ukanda wa Amerika Kusini.

Colombia, inashikilia rekodi ya kusikitisha ya mauaji ya watetezi wa mazingira na 65 waliuawa mwaka jana.

Wengi walilaani unyonyaji mkubwa wa maliasili katika maeneo ambayo makundi yenye silaha mara nyingi yanadhibiti. Watu wa asili wanalengwa hasa na mashambulizi hayo.

Louis Wilson, msemaji wa shirika lisilo la kimataifa la Global Witness, anaelezea kuwa "jamii za watu wa asili zinaathiriwa hasa katika nchi kama Colombia kwa sababu wao ni wasimamizi wa ardhi na wana ulinzi mdogo wa kisheria katika nchi kama Colombia. "

Amerika Kusini, kama vile Asia au Afrika, wanaharakati wa mazingira wanauawa na idadi kubwa ya kesi, hakuna haki yoyote inayotendeka.

Itakumbukwa kwamba mwaka 2017 zaidi ya wanaharakati 200 wa mazingira waliuawa. Mauaji hayo yaliyofadhiliwa na serikali yakihusishwa na miradi mikubwa iliyo na faida kutoka kampuni kubwa ikiongezeka.

"Wakati mahitaji ya bidhaa hizi duniani yakiongezeka, kuna kinyang'anyiro miongoni mwa wafanyabiashara kujipatia kiasi kikubwa cha ardhi wanachohitaji ili kupanda mazao hayo," alisema Ben Leather, mtetezi mwandamizi kutoka Global Witness.

Leather alisema pale watu wanaposimama kudai haki zao na kutaka mazingira yao yalindwe, wananyamazishwa kikatili.

**RFI**

## Dunia yashuhudia joto kali kufikia nyuzi 50

**London, UINGEREZA**

DUNIA inaendelea kushuhudia joto kali kila mwaka wakati joto likifikia nyuzi joto 50 ikiwa ni ongezeko mara mbili, tangu miongo minne kupita.

Ripoti hiyo ni kwa mujibu wa utafiti wa BBC. Pia sasa ni tukio ambalo hutokea katika maeneo mengi zaidi duniani kuliko hapo awali, haijawahi kutokea.

Kati ya mwaka 1980 na mwaka 2009, kiwango cha joto kilipita selsiasi 50 karibu siku 14 kwa mwaka kwa wastani na siku hizo zikaongezeka hadi 26 kwa mwaka kati ya 2010 na 2019.

Katika kipindi hicho hicho, joto kiwango cha selsiasi 45 na zaidi likashuhudiwa kwa wastani wa wiki mbili za ziada kwa mwaka. Ongezeko hilo linahusishwa kwa asilimia 100 na uchomaji wa makaa ya mawe," alisema Dk. Friederike Otto, mwanasayansi anayeongoza katika utafiti wa hali ya hewa.

Pia kuna uwezekano wa joto kuwa kali zaidi kuongezeka.

Joto kali linaweza kuwa hatari kwa mwanadamu na uasilia na kusababisha matatizo makubwa katika majengo, barabara na mifumo ya umeme.

Joto la nyuzi 50 hutokea sana katika maeneo ya Mashariki ya Kati na Ghuba.

Baada ya joto kuvunja rekodi ya nyuzijoto 48.8 za selsiasi huko Italia na nyuzi 49.6 huko Canada, msimu huu wa joto, wanasayansi wameonya kwamba siku za kuwa na nyuzi joto zaidi ya 50 zitaongezeka katika sehemu zingine isipokuwa ikiwa tutasitisha uzalishaji wa nishati ya mkaa ya mawe.

**BBC**

## Mafuriko yaua nchini Sudan

**Khartoum, SUDAN**

MAFURIKO baada ya mvua kubwa kunyesha yamesababisha vifo vya watu zaidi ya 80 na kuharibu maelfu ya nyumba, ofisa wa Sudan amesema juzi.

"Jumla ya watu 84 wameuawa na wengine 67 wamejeruhiwa katika majimbo 11 ya Sudan tangu kuanza kwa msimu wa mvua," amesema Abdel Jalil Abdelreheem, msemaji wa Baraza la kitaifa la Ulinzi wa Raia Sudan.

Vifo hivyo vilitokana na watu kuzama majini, umeme na kuanguka kwa nyumba, alielezea. Baadhi ya nyumba 8,400 zimedondoka na zaidi ya 27,200 zimeharibiwa kote nchini.

Mvua kubwa hunyesha Sudan kati ya mwezi wa Juni na Oktoba na nchi hiyo inakabiliwa na mafuriko makubwa kila mwaka ambayo huharibu mali, miundombinu na mazao. Umoja wa Mataifa (UN), unakadiria kuwa mvua hizo kubwa na mafuriko zimeathiri watu 102,000 tangu Julai.

Karibu vijiji 50 vimesombwa na maji Kusini mwa Sudan na kusababisha watu 65,000 kukosa makazi, ikiwamo wakimbizi wa Sudan Kusini ambao kambi yao imekumbwa na mafuriko.

Mwaka jana, mvua zililazimu mamlaka ya Sudan kutangaza hali ya hatari ya miezi mitatu na ziliathiri watu wasiopungua 650,000 na kuharibu zaidi ya nyumba 110,000.

**RFI**

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499

MECHI KALI

HOME

AWAY



LIVERPOOL

1.51 | 4.51 | 5.62

AC MILAN



1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALE MAJANGA TENA REAL MADRID



**MADRID,** Hispania

UCHUNGUZI wa kimatibabu uliofanywa juzi, umethibitisha kuwa Gareth Bale ameumia kwenye nyama ya mguu wa kulia na atakuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Bale alipata jeraha hilo katika mazoezi ya mwisho ya Real Madrid huko Santiago Bernabeu, Jumamosi kabla ya mechi yao, dhidi ya Celta Vigo Jumapili waliyoshinda kwa mabao 5-2, kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Picha zilisambazwa zikimuonyesha raia huyo wa Wales akijikongoja na bandeji iliyofungwa, kwenye paja lake la kulia baada ya mazoezi.


Jeraha la mshambuliaji huyo limekuja wakati mbaya zaidi kwa Real Madrid, ikizingatiwa ratiba ngumu ya 'Los Blancos' hao kabla ya mapumziko yajayo ya mechi za kimataifa.

Real Madrid ina michezo sita katika wiki tatu zijazo, pamoja na michezo minne kwenye LaLiga na mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kadri Bale umri unavyozidi kusonga mbele amekuwa akiumia zaidi na zaidi kutokana na majeraha, akiugua mara tatu msimu wa 2020/21, akiwa kule Tottenham Hotspur.

Alikuwa nje kwa jumla ya siku 40 kwa shida ya goti, kisha siku 10, kwa sababu ya ugonjwa na siku 18 zaidi, kwa sababu ya jeraha lingine la misuli na sasa anakadriwa atakuwa nje kwa miezi kadhaa.

# CAVANI PANCHA MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

NI muendelezo wa kukosekana kwa Edinson Cavani kwenye kikosi cha Manchester United, kwani majeraha yameendelea kumuweka nje na sasa anatarajiwa kukaa kwa wiki moja au zaidi.

Kwa mujibu wa kocha Ole Gunnar Solskjaer akinukuliwa na vyombo vya habari vya England, baada ya mchezo, dhidi ya Newcastle United kwenye Ligi Kuu England, Cavani alipata jeraha dogo kwenye mazoezi kabla ya mchezo huo na hivyo atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa angalau wiki moja.

Na jana Jumanne aliukosa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, dhidi ya Young Boys ya Uswisi.

Na kwa mujibu wa Sky Sport, Solskjaer anatarajia kumtumia Cavani raia wa Uruguay kuanzia wiki inayokuja na hiyo ikitegemeana na hali yake kama itatengamaa haraka.

Cavani amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na hakuwa na muda mwingi wa kucheza hapo Old Trafford tangu alipowasili kutoka kule PSG.

Licha ya kwamba aliifungua Man United mabao muhimu katika mechi muhimu, lakini hakupata dakika za kutosha za kucheza kutoka na kuwa majeruhi.



## HABARI MICHEZO


,059,740 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 18.9.21 | 17:00 | Derby vs Stoke City | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 2. 18.9.21 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 3. 18.9.21 | 17:00 | Cardiff vs Bournemouth | 2.86 | 3.31 | 2.36 |
| 4. 18.9.21 | 17:00 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 5. 18.9.21 | 18:00 | Lens vs Lille | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 6. 18.9.21 | 19:30 | Aston Villa vs Everton | 2.46 | 3.27 | 2.92 |
| 7. 18.9.21 | 19:30 | Elche vs Levante | 2.67 | 3.13 | 2.77 |
| 8. 18.9.21 | 22:00 | Alaves vs Osasuna | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 9. 19.9.21 | 13:30 | Empoli vs Sampdoria | 2.52 | 3.63 | 2.62 |
| 10.19.9.21 | 14:00 | Nice vs Monaco | 2.73 | 3.38 | 2.48 |
| 11. 19.9.21 | 16:00 | Brighton vs Leicester | 2.83 | 3.19 | 2.58 |
| 12. 19.9.21 | 17:15 | Real Sociedad vs Sevilla | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 13. 19.9.21 | 21:45 | Juventus vs AC Milan | 2.36 | 3.32 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 15 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 1888 | Denizlispor vs Adanaspor | 3.05 | 3.19 | 2.21 |
| 17:00 | 4214 | PS Kemi vs Vifk Vaasa | 4.50 | 4.30 | 1.65 |
| 17:00 | 4461 | Pakhtakor vs Navbahor Namangan | 1.21 | 5.43 | 11.64 |
| 17:00 | 5900 | NK Bednja Beletinec vs NK Osijek | 29.04 | 11.62 | 1.03 |
| 17:30 | 1699 | KPV Kokkola vs EIF Ekenas | 1.93 | 3.49 | 3.44 |
| 17:30 | 2221 | Spartak Moscow vs Legia Warszawa | 1.84 | 3.60 | 4.20 |
| 17:30 | 3216 | Kustosija vs Rudes Zagreb | 2.48 | 3.21 | 2.63 |
| 18:00 | 1321 | Kfum Oslo vs Fredrikstad | 2.25 | 3.54 | 2.72 |
| 18:30 | 1269 | FF Jaro vs RoPs Rovaniemi | 2.26 | 3.33 | 2.85 |
| 18:30 | 3431 | Kapa vs Kiffen | 1.74 | 3.97 | 3.72 |
| 18:30 | 4347 | MP Mikkeli vs Musa Pori | 1.85 | 3.68 | 3.54 |
| 18:30 | 5159 | VPS Vaasa vs Klubi 04 | 1.63 | 3.88 | 4.46 |
| 18:30 | 5323 | TPS Turku vs IF Gnistan | 1.30 | 5.01 | 7.90 |
| 18:45 | 2335 | AL Akhdood vs Bisha FC | 3.13 | 3.13 | 2.19 |
| 19:00 | 1371 | Sandnes Ulf vs Ranheim | 2.87 | 3.70 | 2.10 |
| 19:00 | 2012 | Aalesunds vs Grorud IL | 1.24 | 5.78 | 8.48 |
| 19:00 | 2408 | Jerv vs Aasane Fotball | 1.80 | 3.78 | 3.63 |
| 19:00 | 2473 | Stjordals-Blink vs Strommen | 1.88 | 3.58 | 3.53 |
| 19:00 | 4305 | Flekkeroy vs Kjelsaas | 2.85 | 3.39 | 2.23 |
| 19:00 | 4584 | Fakel vs Yenisey Kr | 1.93 | 3.18 | 3.81 |
| 19:00 | 4722 | Sogndal vs Raufoss | 1.55 | 4.15 | 4.83 |
| 19:00 | 5289 | Torpedo Moscow vs Tom Tomsk | 1.48 | 3.87 | 6.19 |
| 19:00 | 5832 | Ham-Kam vs Bryne | 1.49 | 4.27 | 5.24 |
| 19:00 | 5855 | Tubas vs Shabab Alsamu | 2.13 | 3.25 | 3.15 |
| 19:45 | 2742 | Besiktas vs Borussia Dortmund | 5.18 | 4.39 | 1.56 |
| 19:45 | 3878 | Sheriff Tiraspol vs Shakhtar Donetsk | 4.09 | 3.54 | 1.88 |
| 20:00 | 4647 | Zwickau vs Hallescher | 2.15 | 3.49 | 3.05 |
| 20:15 | 1260 | Union Santa Fe vs Estudiantes LP | 2.94 | 2.80 | 2.51 |
| 21:00 | 3683 | Ullensaker/Kisa vs IK Start | 2.56 | 3.57 | 2.36 |
| 21:45 | 1018 | Birmingham vs Fulham | 3.85 | 3.06 | 2.05 |
| 21:45 | 1532 | Bristol City vs Luton Town | 2.46 | 3.04 | 2.95 |
| 21:45 | 3527 | Stoke City vs Barnsley | 1.76 | 3.40 | 4.73 |
| 21:45 | 4033 | Swansea vs Millwall | 2.60 | 3.00 | 2.80 |
| 21:45 | 4974 | Nottingham vs Middlesbrough | 2.97 | 2.87 | 2.57 |
| 21:45 | 5031 | Coventry vs Cardiff | 2.22 | 3.11 | 3.30 |
| 21:45 | 5483 | Tiverton Town vs Salisbury City | 2.51 | 3.53 | 2.42 |
| 22:00 | 1789 | CD Palestino vs Melipilla | 1.65 | 3.78 | 4.46 |
| 22:00 | 4318 | Atletico Madrid vs Porto | 1.60 | 3.65 | 6.20 |
| 22:00 | 4959 | Manchester City vs RB Leipzig | 1.34 | 5.14 | 8.27 |
| 22:00 | 5228 | Inter vs Real Madrid | 2.42 | 3.54 | 2.75 |
| 22:00 | 5387 | Sporting Lisbon vs Ajax | 2.86 | 3.46 | 2.38 |
| 22:00 | 5532 | Brugge vs Paris St Germain | 9.97 | 5.80 | 1.27 |
| 22:00 | 5817 | Liverpool vs AC Milan | 1.51 | 4.51 | 5.62 |
| 22:15 | 5082 | Grotta vs Afturelding | 1.81 | 4.08 | 3.35 |
| 22:30 | 5425 | Argentinos Juniors vs Patronato Parana | 1.85 | 3.14 | 4.25 |
| 23:00 | 1650 | CD Alianza Cotopaxi vs Chacaritas FC | 2.07 | 3.01 | 3.59 |
| 23:00 | 1712 | AD Grecia vs AD San Carlos | 1.89 | 3.49 | 3.58 |
| 23:00 | 1746 | Puerto Quito vs CD Duros Del Balon | 2.11 | 2.66 | 4.07 |
| 23:00 | 2025 | Gualaceo SC vs Cumbaya FC | 2.26 | 2.86 | 3.30 |
| 23:00 | 4462 | ADR Jicaral vs CS Cartagines | 2.76 | 2.76 | 2.71 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# BARCELONA KUMKOSA BRAITHWAITE HADI 2022

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imethibitisha kwamba, mshambuliaji wake, Martin Braithwaite, atafanyiwa upasuaji wa goti na hiyo itamfanya kukosa mechi zote za kipindi kilichobaki cha mwaka huu wa 2021.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Denmark aliomba kutolewa nje kwenye mchezo wa Barcelona wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Getafe mwezi uliopita kwenye Ligi Kuu baada ya kupata maumivu ya goti na alikosa kuichezea nchi yake kwenye mechi za kimataifa.

Braithwaite awali alionekana kwamba, maumivu hayo ni ya muda mfupi, lakini Barca imethibitisha kwamba atafanyiwa upasuaji ili kuweza kurekebisha goti lake.

"Martin Braithwaite ameumia goti la kushoto na sasa atalazimika kufanyiwa upasuaji," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Raia huyo wa Denmark atafanyiwa upasuaji kwa siku zijazo. Klabu itakuwa ikitoa taarifa hali itakavyokuwa ikiendelea."

Taarifa zaidi zinaeleza kwamba, Braithwaite hatarudi uwanjani kwa kipindi kilichobaki cha mwaka huu, kitu ambacho kitaiacha miamba hiyo ya Catalunya na uhaba wa mshambuliaji.

Ikimbukwe kuwa tayari Barcelona imewatoa Lionel Messi na Antoine Griezmann katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho.

Braithwaite amefunga mabao saba katika mechi 42 kwenye mashindano yote na 'Blaugrana' hao msimu uliopita, kabla ya kufunga mara mbili kwenye mchezo wa ufunguzi wa LaLiga wa ushindi dhidi ya Real Sociedad.



# RICE KUZIGONGANISHA MAN CITY, UNITED

**LONDON, England**

NYOTA wa West Ham United, Declan Rice, ataziingiza kwenye mbio za farasi mmoja, Manchester City na majirani zao wa jiji moja, Manchester United katika usajili ujao baada ya kumkosa kipindi cha dirisha la majira haya ya joto, kwa mujibu wa Daily Mail.

Klabu hizo za Manchester zote zinahitaji kiungo mkabaji na rada zao zilikuwa kwa Rice ambaye klabu yake ilimwekea ngumu.

Pengine United walipaswa kumsajili kiungo wa hulka hiyo kwenye dirisha lililofungwa, lakini haikuwa hivyo, City walipunguza kasi baada ya nahodha wao, Fernandinho kuongeza mkataba wa mwaka mmoja.

Mambo yatakua tofauti kwenye dirisha kubwa la usajili msimu ujao, na tayari klabu yake inayotumia Uwanja wa London, imeshaweka wazi dau la Rice ambalo ni pauni milioni 100.

West Ham waliweka wazi kuwa hawatomuuza Rice kwa dau lolote chini ya pauni milioni 100.

Licha ya kiungo huyo kugoma kusaini mkataba mpya na West Ham, bado amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Rice anaamini 'Wagonga Nyundo' hao wa London walimwekea mazingira magumu ya yeye kusajiliwa msimu huu na hivyo hatosaini mkataba wowote mpya na klabu hiyo, kwani anataka kujiunga na klabu nyingine kubwa zaidi.

Na Man City na United ndizo zenye nafasi kubwa zaidi kupata saini ya nyota huyo na hivyo ripoti hiyo inadai kwamba, zitapigana vikumbo kuwania saini yake kipindi kijacho cha dirisha la usajili.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI YUPO TAYARI KWA UEFA LEO - POCHETTINO

**Tuna matumaini wote wawili tutakuwa na nafasi nzuri ya kufikia mafanikio tunayotaka...**

**PARIS, UFARANSA**

MAURICIO Pochettino amebainisha kwamba, hana maneno mengi ya kuzungumza linapokuja suala la kumwelezea Lionel Messi, lakini amesema mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, ameshazoea mazingira ya Paris Saint-Germain na leo ataanza kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa klabu hiyo.

PSG ilimsajili Messi Agosti baada ya sheria za kifedha kuibana Barcelona, hivyo kushindwa kuendelea naye, na hadi sasa ameichezea dakika 24 timu yake hiyo mpya kwenye mchezo wa ushindi wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Reims kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Messi, ambaye ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne akiwa na Barcelona, leo, Jumatano ataanza kuichezea PSG kwa mara ya kwanza kwenye mashindano hayo dhidi ya Club Brugge, na Pochettino ameiambia UEFA.com kwamba, nyota huyo amejiandaa vizuri.

Wakati alipoulizwa anawezaje kumwelezea raia mwenzake huyo wa Argentina, Pochettino alisema: "Mimi sio mtu sahihi kumwelezea yeye. Kuna watu wengi ambao wana maneno mapana ya kumuelezea yeye kwa kile Leo [Messi] anachostahili.

"Mara zote anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani. Tangu ametua hapa, amezoea haraka sana mazingira na amekuwa akijifua vema kabisa, akijaribu kuwa kwenye ubora wa juu zaidi na naamini muda mfupi tu atakuwa kule anakotaka.

"Sikufikiria kwamba, ingewezekana (asaini kwetu sisi), na wakati nafasi ilipojitokeza kila kitu kilikwenda haraka, na kuna timu ambayo isingeweza kumuacha.

"Hata hivyo, kuna uhusiano, wote mimi na yeye ni Waargentina, wote ni mashabiki wa klabu ya nyumbani ya Newell's (Old Boys), wote tunatoka mji mmoja wa Rosario.

"Nimekuwa navutiwa naye kwa muda mrefu sana wakati nilipokuwa nakabiliana naye kama mpinzani, sasa kuwa naye kwenye kikosi kimoja kwa hakika ni jambo zuri sana kwangu.

"Tuna matumaini wote wawili tutakuwa na nafasi nzuri ya kufikia mafanikio ambayo tunayataka."

## ZISIKUPITE

### POGBA KUONGEZA MKATABA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kujiunga na PSG na Real Madrid, anaelekea kuongeza mkataba katika klabu ya Manchester United baada ya Cristiano Ronaldo kurudi Old Trafford. **(Athletic)**

### BELLINGHAM EURO MIL. 100

KLABU ya Borussia Dortmund ilikuwa inataka euro milioni 100 ili kumruhusu kiungo wake wa kati mwenye umri wa miaka 18, Jude Bellingham kuondoka, huku klabu za Manchester City na Liverpool zikidaiwa kuonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wa England.**(Bild)**

### RICE AWEKEWA BEI

WEST Ham imemwekea bei ya nyota wao, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, ya pauni milioni 100 ili kumuuza kiungo huyo wa England. **(football.london)**

### MOUNT KUPEWA MKATABA

CHELSEA inajiandaa kumpa mkataba mpya kiungo wa England, Mason Mount hatua ambayo huenda ikamfanya mshahara wake kuongezeka hadi kufikia pauni 150,000 kwa wiki**. (90min)**

### TUANZEBE KUBAKI VILLA

NYOTA wa zamani wa Manchester United na England, Axel Tuanzebe mwenye umri wa miaka 23, anataka kuufanya uhamisho wake wa mkopo katika klabu ya Aston Villa kuwa wa kudumu. **(Sun)**

### BAYERN YAMTAKA WERNER

KLABU ya Bayern Munich inataka kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani na Chelsea, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la usajili la Januari. **(Football Insider)**

### LINGARD ATAJWA LEICESTER

LEICESTER City ina nia ya kumsajili kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28. **(Fichajes)**

### CHELSEA NA MABEKI INTER

CHELSEA inawanyatia mabeki wa Inter Milan, Alessandro Bastoni mwenye miaka 22 na raia wa Slovakia, Milan Skriniar, 26. **(Mediaset)**

### SPURS YAJITOSA KWA KASSIE

TOTTENHAM Hotspur, imewasilisha ofa ya kumsajili kungo wa kati wa AC Milan, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 24, ingawa haijulikani iwapo Spurs itawasilisha ombi hilo Januari kumsajili nyota huyo wa Ivory Coast .**(Calciomercato)**

### GOUIRI AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeonyesha nia ya kutaka kumsajili straika wa Nice, Amine Gouiri, huku kocha, Jurgen Klopp akionyeshwa kuvutiwa zaidi na nyota huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21. **(Fichajes)**

### ARSENAL YAMTAKA ISAK

ARSENAL ni moja ya Klabu za Ligi Kuu England zinazomwania straika wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 21. **(Fichajes via FourFourTwo)**

## HABARI MICHEZO

# WALIOKOSA ITC YANGA KUANZIA MAKUNDI CAF

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umethibitisha kupatikana kwa Hati za Uhamisho za Kimataifa (ITC) za wachezaji wake, Fiston Mayele, Shaban Djuma na Khalid Aucho, lakini hawataweza kuwatumia kwenye hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya klabu hiyo, Rodgers Gumbo, alisema tayari wamepata ITC za nyota hao, lakini hawaruhusiwi kuwatumia kwa sasa katika hatua ya awali na hatua ya pili.

"Kwa mujibu wa kanuni na taratibu za CAF (Shirikisho la Soka Afrika), wachezaji hawa hata pale watakapopitishwa rasmi, hatuwezi kuwatumia kwenye hatua hii labda mpaka hatua ya makundi kama tutafanikiwa kufika," alisema Gumbo.

Alisema Wanayanga watulie viongozi wanaweka mikakati kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri na kufika hatua ya makundi kama walivyojiwekea mipango yao.

"Tuna mechi mbili ama tatu muhimu mbele yetu kabla ya kufika hatua ya makundi, tuna mchezo wa marudiano dhidi ya Rivers ya Nigeria, tumepoteza hapa nyumbani, lakini hii si sababu au tiketi ya kuamini kuwa tumetoka. Tuna dakika nyingine 90 ugenini, tumeshaanza kujipanga nazo baada ya mchezo ule wa kwanza kumalizika," alisema Gumbo.

Alisema kamati yake inafanya kazi kwa karibu na uongozi na benchi la ufundi kuhakikisha mambo yanaenda sawa kuelekea kwenye mchezo wa marudiano utakaochezwa Septemba 19, mwaka huu nchini Nigeria.

"Tayari kuna watu wameenda Nigeria kuandaa mazingira mazuri kwa ajili ya timu, na kikosi tunatarajia kiondoke kati ya kesho au keshokutwa Ijumaa, tunaamini mambo yote yataenda sawa," aliongeza kusema Gumbo.

Yanga iliangukia pua kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Rivers United baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 nyumbani, matokeo hayo yanaifanya Yanga sasa kwenda kusaka ushindi wa aina yoyote kuweza kufuzu hatua ya pili ya michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

**KWAHERI...**



Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire (mbele), akiwa amevalia barakoa ya Simba wakati wa kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu wa aliyekuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Simba, Zacharia HansPoppe, juzi, jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Matola aungana na Hitimana, Gomes

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, ambaye kwa muda mrefu hakuwa kwenye kikosi hicho kutokana na kwenda masomoni, amerejea na kuungana na kikosi hicho kilicho kambini jijini Arusha kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa mashindano ndani na kimataifa.

Mratibu wa timu hiyo, Abbas Ally, jana alisema Matola ameungana na kikosi hicho juzi, na kuwakuta Kocha Mkuu Didier Gomes na Msaidizi mpya wa timu hiyo, Thierry Hitimana.

"Kwa sasa kambi imekamilika, wale wachezaji waliokuwa kwenye timu ya taifa, wote wamewasili kambini, sasa tuna wachezaji wote 32 tuliowasajili msimu huu. Halafu tuna makocha wote watatu, hata Matola ambaye alikuwa masomoni, naye ameshawasili kambini kuungana na wenzake, Kocha Mkuu Gomes na Msaidizi Hitimana. Sasa hapa kila kitu kiko vizuri," alisema mraribu huyo.

Alisema kwa sasa wanaendelea na mazoezi, na hata wakicheza mechi za kirafiki hazitokuwa na mashabiki wowote ili kuwapa uhuru wachezaji kufanya kile ambacho kocha anakihitaji, pamoja na kurekebisha makosa.

"Tumekataa mashabiki kwenye mazoezi na mechi zetu ili wachezaji wawe na umakini. Hiki ni kipindi cha maandalizi ya msimu. Makocha wanataka kuangalia nini wanakitengeneza, tuna malengo makubwa sana msimu huu. Msimu uliopita tuliishia robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, safari hii tunataka kufika nusu. Tumepata ubingwa na Kombe la FA, lakini tulilikosa Kombe la Mapinduzi. Sasa haya ni maandalizi muhimu ambayo hatutaki kuyafanyia mchezo.

"Unajua wachezaji nao ni binadamu, kukiwa na mashabiki nao wanakuwa na mihemko, siunajua Simba ina mashabiki wengi sana, hatutaki kuwaondoa wachezaji kwenye umakini hasa wakati huu wa mazoezi ya kuandaa msimu mpya," alisema.

Matola alikuwa anasomea ukocha ili kupata Leseni B ya ukocha, itakayomwezesha kukaa kwenye benchi la timu hiyo kama kocha msaidizi msimu ujao wa ligi.

## Azam kuwakomalia Wasomalia Chamazi

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wanaendelea walipoishia kuhakikisha wanafanya vizuri dhidi ya Horseed SC ya Somalia kwenye mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Bahati alisema hawajamaliza mechi na wanahitaji kupambana zaidi kushinda katika mchezo huo wa marudiano.

Alisema hawabweteki kwa matokeo ya mechi iliyopita na kuona tayari wamemaliza kwa kuwa wanatambua mchezo wa marudiano hautakuwa rahisi kwao.

"Mechi hii ya marudiano itakuwa ya ushindani na ugumu kuliko ya kwanza kwa sababu tunaenda kukutana kila mmoja wetu anafahamu mbinu za mwenzake," alisema Bahati.

Azam FC watakuwa ugenini katika mchezo huo wa marudiano utakaopigwa katika Dimba la Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam badala ya Uwanja wa Uhuru kama ilivyotangazwa awali.

## Yosso wenye vipaji waitwa kliniki Moro

**Na Paulina Chimeledya, TUDARCo**

VIJANA wenye vipaji vya soka nchini wametakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye kliniki maalum ya kung'amua vipaji vya mchezo huo iliyoanza jana katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kikundi, Manispaa ya Morogoro.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa wiki iliyopita na Mwalimu wa soka, Boniface Kiwale, ambaye ni Meneja wa Moro Soka Academy, vijana wote wenye vipaji ambao wana umri chini ya miaka 15 ndio wanaohitajika katika kliniki hiyo.

Aidha, ilieleza kuwa watakaochaguliwa katika kliniki hiyo watapata fursa ya kwenda kujiunga na Moro Soka Academy kupata elimu na kuendeleza vipaji vyao.

"Kliniki hii ni ya wazi na itafanyika ndani ya wiki moja, lengo ni kuangalia wachezaji wenye vipaji ili kuweza kuwajumuisha kwenye vituo vyetu, " Kiwale alieleza katika taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa, vijana wenye nia ya kushiriki katika kliniki hiyo wanapaswa kufika eneo la tukio kwa gharama zao wakiwa na chupa ya maji na vifaa vya michezo.

# Michezo

Jumatano Septemba 15, 2021

Nipashe




Messi yupo tayari kwa Uefa leo - Pochettino

UKURASA 22

# RIVERS UNITED YAITISHA YANGA 'KUFIA' NIGERIA

## ●●●Yaitangazia nne, yatafuta pumzi kwa Enyimba, wenyewe kuifuata Ijumaa na mashabiki 48 huku...

**Tunu Hassan, TUDARCo**

WAKATI wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika walioanzia hatua ya awali, Yanga, wakitarajia kuondoka nchini Ijumaa kwenda Nigeria tayari kwa mchezo wa marudiano dhidi ya Rivers United ya huko, wapinzani wao hao wamejigamba watawapiga si chini ya mabao manne.

Timu hizo zinatarajia kurudiana Jumapili, Yanga ikihitaji ushindi zaidi ya bao moja ili kusonga mbele baada ya ule wa awali, Uwanja wa Benjamin Mkapa mwishoni mwa wiki kukubali kipigo cha bao 1-0.

Akizungumzia mechi hiyo ya marudiano, Ofisa Habari wa Rivers United, Charles Mayuku, alisema wanatambua itakuwa ngumu na leo ama kesho wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Enyimba kujiandaa na mchezo huo ambao kwao wanahitaji ushindi ama sare yoyote ili kusonga mbele. "Tumefika salama nyumbani na leo au kesho tunatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Enyimba. Wachezaji wetu wanne na viongozi watatu waliokutwa na corona wako salama na hakuna mwenye maambukizi, nadhani zilikuwa mbinu chafu za wapinzani wetu.

"Bado wageni wetu (Yanga) hawajatupa taarifa ni lini wanatarajia kuwasili nchini (Nigeria), lakini tumejipanga kuwapokea kama walivyotupokea," alisema Mayuku.

Naye mmoja wa maofisa wa timu hiyo, alinukuliwa akiiponda Yanga akisema: "Wanacheza kama watoto, hawatuwezi walitumia COVID-19 kuwaondoa wachezaji wetu wanne bora tena muhimu, kipa wetu namba moja hakucheza, isitoshe wachezaji wetu watatu wa muhimu, washambuliaji hawakucheza waliwaondoa.

"Sisi tuna timu nzuri, tulijiandaa nao, tulijua watafanya huu mchezo kwa hiyo tukawa tayari kwa ajili yao kila kona, lakini nimeshangazwa sana kwa walichotufanyia, walitupiga kumnasa vibao ofisa wetu, hii si sawa sisi ni wamoja sisi sote ni Waafrika, mpira ni urafiki ni mchezo wa uungwana.

"Sasa tumeshinda 1-0 licha ya vitisho vyote hivyo, watakuja tu kule Port Harcourt Nigeria, wakija tutawachukulia kama ndugu zetu ila tutawafunga si chini ya mabao 4-0, tutawapa 4-0 mtayasikia tu matokeo.

"Hawa hamna kitu ni watoto sana, ni wadogo sana, unaweza kuona mchezo tulicheza nao, hawa hamna kitu, watakuja Nigeria tutawapigia mpira mwingi."

Kwa upande wa uongozi wa Yanga, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema timu hiyo inatarajia kwenda Nigeria Ijumaa kwa ndege ya kukodi ya Air Tanzania na wametoa nafasi ya mashabiki 48.

"Tutaondoka Ijumaa na ndege ya kukodi ya Air Tanzania, tumetoa nafasi kwa mashabiki 48 ambao watakuwa kwenye msafara wa timu, na kwamba wanachotakiwa ni kuchangia dola 1,200 kama gharama ya kwenda na kurudi, VISA na vipimo vya COVID-19," alisema Bumbuli.

Kuhusu hali ya kikosi, Bumbuli alisema maandalizi yanaendelea vizuri na mshambuliaji Hetier Makambo ambaye aliumia anaendelea vizuri na anatarajiwa kuwa sehemu ya wachezaji watakaosafiri na timu.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya klabu hiyo, Rodgers Gumbo, alisema Wanayanga watulie viongozi wanaweka mikakati kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri na kufika hatua ya makundi kama walivyojiwekea mipango.

"Tuna mechi mbili ama tatu muhimu mbele yetu kabla ya kufika hatua ya makundi, tuna mchezo wa marudiano dhidi ya Rivers ya Nigeria, tumepoteza hapa nyumbani, lakini hii si sababu au tiketi ya kuamini kuwa tumetoka. Tuna dakika nyingine 90 ugenini, tumeshaanza kujipanga nazo baada ya mchezo ule wa kwanza kumalizika," alisema Gumbo.

TUPO TAYARI...




Wachezaji wa Yanga wakiendelea na mazoezi katika kambi ya timu hiyo, Avic Town, Kigamboni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

## Mazembe yaanika 23 wakuivaa Simba J'Pili

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa Simba ukieleza kuanzia leo, Jumatano wataanza utaratibu wa kuchangia damu, kuelekea tamasha la klabu hiyo maarufu Simba Day, wapinzani wao watakaokuja kucheza mechi ya kirafiki, TP Mazembe ya DR Congo, wameanika majina ya wachezaji 23 watakaokuja Jumamosi kucheza mechi ya kirafiki na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara Jumapili wiki hii.

Simba ambayo jana ilicheza mechi ya kirafiki jijini Arusha dhidi ya Aigle Noir ya Burundi na kushinda 2-1, inatarajia kufanya tamasha hilo Jumapili wiki hii, ambalo ni maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wao wa msimu mpya na siku hiyo ikihitimisha kwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya TP Mazembe.

Akizungumzia maandalizi ya tamasha hilo jana, Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ezekiel Kamwaga, alisema kuanzia leo watatangaza maeneo na vituo watakavyoenda kutoa msaada wa kuchangia damu kuelekea Simba Day.

"Kwa Zanzibar tutakuwa na zoezi la kuchangia damu katika Hospitali ya Mnazimmoja sehemu inayohudumia kinamama wajawazito. Mwaka huu tunaangalia sana kinamama wajawazito na watoto, pia kutakuwa na shughuli nyingine za kijamii ambazo tutakuwa tunazitangaza," alisema Kamwaga.

Wakati Kamwaga akieleza hayo, TP Mazembe imetaja majina ya wachezaji 23 watakaokuja kuunda kikosi cha kuivaa Simba kuwa ni; Mounkoro Ibrahim, Saidi Ngusia Baggio, Ochaya Joseph Benson, Atibu Radjabu Johnson, Issama Mpeko Djos, Masengo Yumba Godet, Tandi Mwape, Luzolo Nsita Ernest na Mundeko Zatu Kelvin.

Wengine ni Kouame Koffi Raoul, Zemanga Soze, Kalaba Rainford, Mayombo Etienne Raby, Sudi Bibonge Gondry, Mika Michee, Kinzumbi Phillippes Beni, Ngimbi Vumbi Merceil, Bileko Mbaki Kelvin, Baleke Othos Jean, Beya Tumuteka Joel, Ntambwe Kolonji Magloire na Zola Kiaku


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >